LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU



# MUHTASARI WA RIPOTI YA HAKI ZA BINADAMU 2021

## Wito wa Kufanya Maboresho ya Mfumo wa Haki Jinai Kulinda Haki za Binadamu



## WAANDISHI, WAHARIRI NA WACHAPISHAJI


**Waandishi:**
Bw. Fundikila Wazambi
Bi. Victoria Lugendo

**Wahiriri:**
Ms. Anna Henga
Ms. Felista Mauya



**Mchapishaji:**
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu
Aprili 2022


HAKIUZWI


**Namba ya Kijitabu(ISBN):**
**978-9987-740-65-9**

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| **Kuhusu Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu** | **iii** |
| **Utangulizi** | **iv** |
| **SURA YA KWANZA:** Utangulizi | **01** |
| **SURA YA PILI:** Haki za Kiraia na Kisiasa | **07** |
| **SURA YA TATU:** Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni | **27** |
| **SURA YA NNE:** Haki za Kiujumla | **35** |
| **SURA YA TANO:** Haki za Makundi Maalum | **39** |
| **SURA YA SITA:** Mifumo ya Ulinzi wa Haki za Binadamu | **63** |
| **SURA YA SABA:** Utekelezaji wa Mapendekezo kwenye Ripoti Zilizopita za Haki za Binadamu | **67** |
| **SURA YA NANE:** Hitimisho na Mapendekezo | **70** |

# KUHUSU KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ni shirika binafsi, huru, la hiari, lisilo la kiserikali, lisilofungamana na chama chochote cha kisiasa na lisilotengeneza faida kwa ajili ya kugawana, ambalo linalenga kufikia jamii yenye haki na usawa. LHRC ina lengo la kuwawezesha Watanzania kukuza, kuimarisha na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini. Lengo kubwa la LHRC ni kujenga ufahamu wa sheria na haki za binadamu miongoni mwa umma na hasa watu walio kwenye hatari kubwa ya kunyimwa haki zao za msingi, kutoa elimu ya sheria na uraia, kufanya utetezi unaohusisha pia msaada wa kisheria, utafiti na ufuatiliaji wa haki za binadamu. LHRC ilianzishwa mwaka 1995 na inafanya kazi Tanzania Bara.

# UTANGULIZI

- Tanzania yapata Rais wa kwanza mwanamke – habari njema kwa ushiriki wa wanawake katika siasa na uwakilishi katika vyombo vya ufanyaji maamuzi.
- Ombi la Rais Samia: Kasi ya uchunguzi wa kesi za jinai iongezeke kulinda haki za watuhumiwa.
- Wito wa viongozi wa juu Serikalini, akiwamo Rais wa nchi na wadau wengine, wa kufanyika kwa maboresho ya haki jinai ili kutatua changamoto za mfumo wa haki jinai nchini.
- Wasichana waliopata ujauzito na waliokuwa na watoto kuruhusiwa kuendelea na shule baada ya Serikali kuleta sera ya kuwarejesha katika mfumo rasmi wa elimu.
- Wito wa wadau wa kuondolewa kwa adhabu ya kifo.
- Kuongezeka kwa matukio ya ukatili dhidi ya mwenza na mauaji yanayofanywa na mwenza.
- Kuripotiwa matukio mengi ya ukatili dhidi ya watoto, ikiwemo ukatili wa kingono na usafirishaji haramu wa watoto.
- Marekebisho ya Kanuni za Maudhui ya Mtandao na Kanuni za Redio na Televisheni.
- Rais Samia kuweka rekodi mpya baada ya kuteua Majaji wapya 28, wakiwemo Majaji wa Mahakama ya Rufani 7.
- Mapendekezo ya dhamana kutolewa kwa makosa yote, kama ilivyo katika nchi jirani ya Kenya, lakini Mahakama ikiwa na maamuzi ya mwisho kuhusu utoaji wa dhamana kwa kila kesi.
- Kuongezeka kwa wasiwasi miongoni mwa wanajamii na wadau kuhusu watuhumiwa kukaaa rumande/jela mruda mrefu kabla ya kesi kuanza kusikilizwa rasmi.
- Wito wa kufanya maboresho ya mfumo wa haki jinai kwa watoto.
- Kutengenezwa kwa Mpango Kazi mpya wa Kutokomeza Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa mwaka 2021-2024.
- Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu kuifanyia Tanzania tathmini ya haki za binadamu kwa mara ya tatu tangu utaratibu huo wa kufanyia nchi tathmini kuanzishwa.
- Uteuzi wa viongozi wanawake katika nafasi nyeti katika Baraza la Mawaziri.
- Uzinduzi wa Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza katika Afya na Maendeleo kwa Vijana Balehe (2021/22- 2024/25)
- Mkakati wa Taifa wa Haki Jinai ya Mtoto (2020/21 – 2024/25) kupitishwa na Wizara ya Katiba na Sheria mwezi Machi mwaka 2021.
- Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu kuthibitisha na kutamka rasmi kwamba haki ya mazingira safi na yenye afya ni haki ya binadamu.

# DONDOO MUHIMU KWA MWAKA 2021

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Haki Jinai | ▪ Watuhumiwa wa makosa ya jinai wanaweza kukaa gerezani zaidi ya miaka 6 wakisubiri kesi kuanza rasmi baada ya uchunguzi kukamilika.<br>▪ Wafungwa na mahabusu wanawake wanaathiriwa zaidi na mazingira mabaya au yasiyoridhisha ya gerezani.<br>▪ Tabia za kihalifu kwa upande wa wanawake zinachangiwa zaidi ya ukatili au unyanyasaji wa kihisia, kimwili, na/au kingono waliopitia huko nyuma katika Maisha yao.<br>▪ Madhara ya kuwaweka kuzuizini kwa muda mrefu wanawake waliovunja sheria ni makubwa zaidi kwa watoto wanaofungwa nao au waliowaacha nje. |
| 2 | Mauaji yanayofanywa na mwenza | ▪ Asilimia kubwa ya wahanga wa mauaji yanayofanywa na mweza ni wanawake.<br>▪ Kwa mwaka 2021, karibia watu 9 kati ya 10 waliouwawa na wenza wao walikuwa wanawake. |
| 3 | Madhara ya Uviko19 | ▪ Janga la Uviko19 liliathiri sana utekelezaji na ufurahiaji wa haki za binadamu mwaka 2021, hasa haki za kiuchumi na kijamii.<br>▪ Kiujumla, wanawake na watoto waliathiriwa zaidi na janga la Uviko19. |
| 4 | Wosia | ▪ Ni Mtanzania 1 kati ya 10 pekee ameandika wosia.<br>▪ Mtazamo wa watu wengi, hasa walio vijijini na mijini, ni kwamba kuandika wosia ni kujichulia kifo. |
| 5 | Usafirishaji haramu wa binadamu | ▪ Mwaka 2021 Tanzania ilibakia katika nafasi yake ya 124 katika Viwango vya Uhuru wa Vyombo vya Habari vya mwaka 2021, sawa na mwaka 2020. Tanzania ilifikia nafasi hiyo baada ya kushuka kwa nafasi 31 kati ya mwaka 2018 hadi 2020. |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Usafirishaji haramu wa binadamu | ▪ Wahanga wakubwa wa usafarishaji haramu wa binadamu ni wanawake na wasichana.<br>▪ Katika nchi za Kusini mwa Janga la Sahara, ikiwemo Tanzania, watoto wamekuwa wakisafirishwa kwenda kufanya kazi katika mashamba, migodi na sehemu za kuponda mawe, na mitaani, ambapo hutembeza na kuuza bidhaa.<br>▪ Watoto wa kike na wanawake wanaosafirishwa kwa ajili ya kufanya kazi za majumbani hupatwa na madhara makubwa. |
| 7 | Haki za wajane | ▪ Kutolewa kinguvu nyumbani na kunyang'anywa mali ni changamoto kubwa kwa wajane na watoto wao.<br>▪ Marekebisho ya kisheria yanahitajika kulinda haki za wajane za kumiliki mali na kupata urithi. |
| 8 | Ukatili dhidi ya wazee | ▪ Wazee katika sehemu mbalimbali nchini wamedai kuishi katika hali ya kuogopa kushambuliwa na watoto wao, hasa wa kiume, sababu ya kudai mali au urithi.<br>▪ Idadi kubwa ya wa wahanga wa mauaji yanayotokana na Imani za kishirikina ni wazee, hasa wazee wanawake. |
| 9 | Afya ya akili | ▪ Asilimia kubwa ya wahanga wa kujiua (42%) ni vijana.<br>▪ Watu 4 kati ya 10 waliojiua mwaka 2021 walikuwa ni vijana (miaka 15-35). |
| 10 | Ukatili dhidi ya watoto | ▪ 89% ya matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyoripotiwa na vyombo vya habari mwaka 2021 yalikuwa ni ya ukatili wa kingono.<br>▪ Matukio mengi ya wazazi/walezi kuwaunguza watoto wao mikono kama adhabu baada ya kukosea yaliripotiwa mwaka 2021. |

# HAKI 5 ZILIZOKIUKWA ZAIDI MWAKA 2021

**01**

**Haki ya Kuishi**
*[Mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi; Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina; Watu kupotelea kusikojulikana; Ukatili na mauaji yanayofanywa na mwenza]*

**02**

**Uhuru dhidi ya Ukatili**
*[Ukatili dhidi ya wanawake na watoto; Ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu na wazee]*

**03**

**Haki ya Usawa mbele ya Sheria**
*[Kuwekwa kuzuizini kwa muda mrefu; Vikwazo vya ufikiaji haki m.f. rushwa]*

**04**

**Haki ya kuwa Huru na Salama**
*[Uwekwaji kuzuizini gerezani kwa muda mrefu kusubiria kesi;Kukataliwa dhamana; Ukatili dhidi ya wanawake na watoto; Ukamataji na uwekaji kuzuizini watu kinyume na sheria; Ubambikaji wa kesi]*

**05**

**Uhuru wa Kujieleza**
*[Ukamataji na uwekaji kuzuizini watu kinyume na sheria; Unyanyasaji wa wanahabari; Sheria na kanuni zenye vifungu vinavyominya uhuru wa vyombo vya habari na wanahabari]*

# MADHUMUNI YA RIPOTI NA MBINU ZA UKUSANYAJI WA TAARIFA

## MADHUMUNI

**Elimu ya haki za binadamu**
– Haki fulani inamaanisha na kujumuisha nini? Haki hiyo inalindwa na mfumo upi wa kisheria? Kwa nini haki hii ni muhimu? Haki hii ina mipaka ipi?

**Kukumbushia**
– ni maeneo gani ya haki za binadamu yanahitaji kuimarishwa?

**Uchechemuzi wenye ushahidi**
– nini kinahitaji kubadilika na kwa nini?

**Mambo na matukio yaliyosaidia ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu**
- ni mambo au matukio gani yameimarisha ulinzi au utekelezaji wa haki za binadamu?

**Mambo na matukio yaliyoathiri ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu**
– ni mambo au matukio gani yameathiri ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu?

**Uchambuzi wa sheria na miswada**
– ni nini kimebadilika kufuatia utungwaji wa sheria au marekebisho ya sheria au kanuni? Mabadiliko hayo yameleta au yataleta athari gani kwenye haki za binadamu?

**Mapendekezo**
– nini kifanyike kuimarisha na kulinda haki za binadamu?

**Utoaji taarifa**
– kutoa taarifa kuhusu haki za binadamu na masuala ya kisheria ili kuchukua tahadhari na kutekeleza wajibu kwa mujibu wa sheria mbalimbali za nchi.

**Kuonyesha mienendo**
– hali ilikuwaje miaka ya nyuma ukilinganisha na sasa?

**Kutoa mwanga katika kupanga afua**
– ripoti inaweza kutumika kama sehemu ya kuanzia katika kupanga afua mbalimbali.

**Kuelemisha**
– kutoa elimu kuhusu haki za binadamu; elimu kuhusu mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu ya kitaifa, kikanda na kimataifa; elimu kuhusu masuala ya kisheria; elimu kuhusu mambo mapya kuhusu sheria na haki za binadamu.

# MBINU ZA UKUSANYAJI TAARIFA

Taarifa zilizotumika kuandaa Ripoti hii zilipatikana kupitia vyanzo vya awali na upili. Taaria za awali zilipatikana kupitia Utafiti wa Haki za Binadamu 2021, ambao ulifanyika katika mikoa 20 ya Tanzania Bara; shughuli za Kituo na huduma kwa wanufaika wa huduma hizo; na programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu. Taarifa za upili zilipatikana kupitia mapitio ya vyanzo mbalimbali vya kuamikina vya taarifa, ikiwemo Ripoti za wadau wa kiserkali na wasio wa kiserikali. Pia, utafiti wa LHRC wa taarifa zilizotolewa na vyombo vya habari kwa mwaka 2021 ulitoa taarifa muhimu zilizosaidia uandaaji wa ripoti hii ya haki za binadamu, ikiwemo kuwezesha ufanyaji wa utafiti zaidi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na sheria na haki za binadamu yaliyojitokeza katika taarifa hizo.

# KUHUSIANA NA RIPOTI

Ripoti ya Haki za Binadamu ya mwaka 2021 ni Ripoti ya 20 kuandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu tangu kilipoanzisha utaratibu huo mwaka 2002. Ripoti ya mwaka huu imeangazia hali ya haki za binadamu kwa pande zote mbili za Tanzania, yaani Tanzania Bara na Zanzibar.Sehemu ya Kwanza ya Ripoti inagusia hail ya haki za binadamu kwa upande wa Tanzania Bara, huku Sehemu ya Pili ikigusia hali ya haki za binadamu kwa upande wa Zanzibar. Ripoti imefanya tathmini ya hali ya haki za binadamu nchini kulingana na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, na inajumuisha vizazi vyote vitatu vya haki za binadamu, ambavyo ni: haki za kiraia na kisiasa; haki za kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni; na haki za kiujumla.

| | |
|---|---|
| **SURA YA KWANZA:** Utangulizi | Inaelezea kwa kifupi kuhusu Tanzania, ikigusia historia, jiografia, idadi ya watu na mihimili ya serikali, na wajibu wa mihimili hii katika ulinzi wa haki za binadamu. |
| **SURA YA PILI:** Haki za Kiraia na Kisiasa | Inaelezea hali ya haki za msingi za kiraia na kisiasa, ikiwemo uhuru wa kujumuika na kukusanyika; uhuru wa kujieleza; haki ya usawa mbele ya sheria na kupata nafuu ya kisheria; haki ya kuishi. |
| **SURA YA TATU:** Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni | Inaelezea haki muhimu za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, ikiwemo haki ya kufanya kazi, haki ya elimu, haki ya afya na haki ya maji safi na salama.. |
| **SURA YA NNE:** Haki za Kiujumla | Inaangazia hali ya haki za kiujumla, hususan haki ya maendeleo na haki ya kufurahia na kufaidika na rasilimali asilia/maliasili. |
| **SURA YA SITA:** Haki za Makundi Maalum | Inaelezea hali ya haki za wanawake, watoto, watu wenye ulemavu, wazee, watu wanaoishi na VVU, vijana, na wakimbizi. |
| **SURA YA SITA:** Mifumo ya Ulinzi wa Haki za Binadamu | Inaangazia mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu katika ngazi za kitaifa, kikanda, na kimataifa na kujadili wajibu wake katika ulinzi wa haki za binadamu. |
| **SURA YA SABA:** Utekelezaji wa Mapendekezo katika Ripoti Zilizopita | Inafanya tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti zilizopita za haki za binadamu. |
| **SURA YA NANE:** Hitimisho na Mapendekezo | Inatoa hitimisho kuhusu haki za binadamu na kutoa mapendekezo yatakayosaidia kukuza na kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu nchini Tanzania. |



01

SURA YA KWANZA:

# UTANGULIZI

SURA YA KWANZA:

# UTANGULIZI

## 1.1. Historia

Kabla ya kutawaliwa na wakoloni wa Kijerumani na Kiingereza katika Karne ya 19, Tanganyika (sasa Tanzania Bara) ilikaliwa na wazawa waliokuwa wakizungumza lugha ya Kibantu, ambao baadaye walipata ugeni toka Bara la Asia na toka Uarabuni. Kufikia Karne ya 15 Wareno nao wakaingia; na katika kipindi hicho cha Waarabu na Wareno ndipo biashara ya utumwa ilipamba moto. Ilipofika mwaka 1880 ulifanyika mkutano mkubwa katika Mji wa Berlin – Ujerumani, ambapo nchi za Ulaya zililigawa Bara la Afrika kwa ajili ya kulitawala. Ujerumani ilipewa sehemu mbalimbali za Afrika Mashariki, ikiwemo Tanganyika. Baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, Tanganyika iliwekwa chini ya ukoloni wa Uingereza, mpaka ilipofikia mwaka 1961, ambapo Tanganyika ilipata uhuru. Katika kipindi chote cha ukoloni, machifu mbalimbali walipigana na uongozi kandamizi wa kikoloni, **ambao ulikandamiza haki zao kama binadamu**, akiwemo Mtemi Mirambo wa Wanyamwezi, Mangi Meli wa Wachagga na Abushri wa Pangani. Mapigano makubwa zaidi yalitokea Mwaka 1905 wakati wa ukoloni wa Mjerumani, yakifahamika zaidi kama Vita vya Majimaji, ambavyo viliongozwa na kiongozi wa kimila na kiroho aliyeitwa Kinjekitile Ngwale, ambaye aliaminika kuwa na uwezo wa kugeuza risasi kuwa maji.

Harakati za kupata uhuru ziliongozwa na chama cha TANU (Tanganyika African National Union), ambacho kilizaliwa mwaka 1954, kabla ya hapo kikifahamika kama TAA (Tanganyika African Association), kilichoanzishwa mwaka 1929. Kiongozi wa chama alikuwa Mwl. Julius Nyerere, ambaye aliiongoza TANU na Tanganyika kupata uhuru mwaka 1961, akiwa Waziri Mkuu wa Kwanza chini ya **Katiba ya Uhuru**. Mwaka 1962, Tanganyika ikawa Jamhuri, Nyerere akiwa Rais wake wa kwanza chini ya **Katiba ya Jamhuri**, ambayo ilimfanya kuwa Kiongozi wa Taifa, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu, pia akiwa sehemu ya Bunge. Mwaka 1964, Tanganyika

iliungana na Zanzibar, ambayo ilikuwa imepata uhuru toka kwa Sultani wa Oman mwaka 1963, na kuunda Tanzania. Katiba ya tatu, **Katiba ya Muungano**, iliundwa, ikileta mfumo wa serikali mbili, chini ya vyama vya TANU (Tanzania Bara) na ASP (Zanzibar). Mwaka 1965, Katiba ya Mpito iliundwa, ambayo ilirudisha nchi katika mfumo wa chama kimoja. Katiba hii ilipitishwa kama sheria nyingine za bunge, kinyume na kanuni za kikatiba. Mwaka 1977, vyama vya siasa vya TANU na ASP viliungana na kuunda Chama cha Mapinduzi (CCM), ambacho kilitengeneza **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ya mwaka 1977, ambayo ndio inayotumika mpaka leo, japo imekuwa ikifanyiwa marekebisho mbalimbali yapatayo kumi na nne mpaka mwaka 2015. Mojawapo ya marekebisho makubwa ni yale ya mwaka 1992, ambayo yalirudisha mfumo wa vyama vingi. Mengine ni yale ya mwaka 1984, ambayo hatimaye yaliingiza hati ya haki za binadamu kwenye Katiba. Kabla ya hapo, tangu nchi ipate uhuru, haki za binadamu hazikuonekana kuwa muhimu sana kuwekwa kwenye Katiba, japo Tanzania ilikuwa imeshaanza kuridhia baadhi ya mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu.

## 1.2. Jiografia

Tanzania iko kati ya Latitudo 10 na 120 Kusini na Longitudo 290 na 410 Mashariki. Inapakana na Bahari ya Hindi upande wa Mashariki na imepakana na nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi na Zambia kwa pande nyingine. Tanzania ndio nchi kubwa kuliko zote Afrika Mashariki na ina Mlima Kilimanjaro, ambao ndio mlima mrefu kuliko yote barani Afrika, wa tatu duniani. Tanzania imebarikiwa kuwa na maliasili nyingi, ikiwemo mimea, mabonde ya ufa, maziwa, mito na mbuga za wanyama. Maziwa ni pamoja na Ziwa Victoria - ambalo ni kubwa kuliko yote Afrika, na Ziwa Tanganyika - ambalo lina kina kirefu kuliko yote Afrika. Mbuga za wanyama ni pamoja na Serengeti, Mikumi, Manyara, Ngorongoro na Katavi.

## 1.3. Idadi ya Watu

Idadi ya watu Tanzania inaendelea kuongezeka, ambapo kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, idadi ya watu ni **43,625,354** kwa Tanzania Bara na **1,303,569** kwa Zanzibar. Wanawake ni wengi zaidi (51.3%) ikilinganshwa na wanaume (48.7%). Kufikia mwaka 2016, idadi ya watu iliongezeka hadi kufikia takribani **50,144,175**, huku **24,412,889** wakiwa wanaume na **25,731,286** wakiwa wanawake. Idadi kubwa ya watu wapo vijijini kuliko mijini.

## 1.4. Mihimili ya dola na wajibu wa mihili hiyo katika ulinzi wa haki za binadamu

Kuna mihimili mikuu mitatu ya dola nchini Tanzania, ambayo ni: Serikali, Bunge na Mahakama. Mihimili hii imeanzishwa na kupewa mamlaka na Katiba **ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.**

### A. Serikali Kuu

Serikali inajumuisha Rais - ambaye ni Kiongozi wa Taifa, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu - na Baraza la Mawaziri. Baraza la mawaziri linajumuisha Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Rais wa Zanzibar na mawaziri wote. Rais ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri. Makamu wa Rais anamsaidia Rais kwenye mambo yote ya muungano. Zanzibar ina serikali yake na Rais wake chini ya mfumo wa serikali mbili ambao Tanzania inautumia, na ina mamlaka juu mambo yote ambayo siyo ya muungano, kama yalivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***Wajibu katika ulinzi wa haki za binadamu:*** Wajibu wa Serikali Kuu ni pamoja na kutekeleza majukumu yake chini ya mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia; kuilinda Katiba, ambayo inajumuisha haki za binadamu; kuhakikisha utekelezaji wa haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kwa kutoa huduma za kijamii kama vile maji, afya na elimu; kulinda haki ya kuwa huru na salama kupitia vyombo vya dola na mifumo ya haki; kutuoa ulinzi wa kisheria na wa haki za binadamu kupitia Jeshi la Polisi, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na wizara husika katika sekta mbalimbali.

**IDADI YA WATU TANZANIA**



**SENSA YA 2012**

IDADI YA WATU
43,625,354
TANZANIA BARA
1,303,569
ZANZIBAR

WANAWAKE 51.3%

WANAUME 48.7%

**MAKADIRIO 2016**

MAKADIRIO YA IDADI YA WATU
50,144,175

WANAUME
24,412,889

WANAWAKE
25,731,286

### B. Bunge

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo chombo kikuu cha kutunga sheria nchini, ambacho kinaundwa na wabunge mbalimbali wa chama tawala na vyama vya upinzani. Rais pia ni sehemu ya Bunge kwa mujibu wa Katiba. Kazi kuu ya bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali. Bunge hili lina mamlaka juu ya mambo yote ya muungano. Zanzibar ina Baraza la Wawakilishi, ambalo ndiyo chombo chake kikuu cha kutunga sheria na kuisimamia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Bunge lina wabunge wa kuchaguliwa na wabunge wa kuteuliwa.

***Wajibu katika ulinzi wa haki za binadamu:***
Utungaji wa sheria za kulinda haki za binadamu; uridhiaji wa mikataba na utungaji wa sheria za kusaidia utekelezaji wa mikataba hiyo; kuisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa shughuli zake; kujadili masuala mbalimbali yanayohusiana na haki za binadamu na kuyatolea maamuzi.

**Marais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Mw. Julius Kambarage Nyerere: 1964-1985
Ali Hassan Mwinyi: 1985-1995
Benjamin William Mkapa: 1995-2005
Jakaya Mrisho Kikwete: 2005-2015
John Pombe Magufuli: 2015- 2021
Samia Suluhu Hassan – 2021 mpaka sasa

### C. Mhimili wa Mahakama

Mahakama ni chombo kikuu cha utoaji haki nchini Tanzania, ambapo kuna mahakama kadhaa ambazo zinatofautiana kimamlaka. Mahakama ya juu kabisa ni Mahakama ya Rufaa, ambayo ina majaji wa Mahakama ya Rufaa, ambao husimamia na kutolea maamuzi kesi zote za rufaa. Ya pili ni Mahakama Kuu, ambayo pia ina majaji (Majaji wa Mahakama Kuu), ambao husimamia kesi zote katika ngazi hiyo na kuzitolea maamuzi. Mahakama zinazofuatia ni Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo – ambayo ndiyo mahakama ya chini kabisa. Tofauti na Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu, mahakama hizi za chini zina mahakimu. Mahakama Kuu ina vitengo mbalimbali, ikiwemo cha ardhi, biashara, kazi na cha rushwa – ambacho kiliundwa mwaka 2016. Majaji wanateuliwa na Rais baada ya kupata ushauri wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, huku mahakimu wakichaguliwa na Tume hiyo moja kwa moja. Pia kuna Mahakama Maalum ya Katiba, ambayo ina mamlaka ya kushughulikia kesi za kikatiba, ikiwemo haki za binadamu. Ukiacha mahakama hizi, kuna mahakama za kijeshi-ambazo ni mahsusi kwa ajili ya wanajeshi.

Mahakama ya Rufaa ni mahakama yenye mamlaka hadi Zanzibar, ambayo pia ina mahakama zake ziitwazo Mahamaka Kuu ya Zanzibar, Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo. Pia kuna Mahakama ya Rufaa ya Kadhi na Mahakama ya Kadhi.

***Wajibu katika ulinzi wa haki za binadamu:*** Mhimili huu una wajibu mkubwa katika ulinzi wa haki za binadamu, ikiwemo kutafsiri sheria mbalimbali, ikiwemo zinazohusu haki za binadamu; kuchukua hatua za kisheria dhidi ya watuhumiwa wa vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu; na kusikiliza madai yanayohusiana na haki za binadamu. Mhimili huu pia hufanya mapitio ya maamuzi na vitendo vya watu na mamlaka mbalimbali kulingana na viwango vya haki za binadamu; huimarisha upatikanaji wa haki; hukuza utaratibu wa kisheria; na hutunga sheria kupitia kesi.

**Hali ya Haki za Binadamu Kiujumla kwa mwaka 2021**

Kulingana na tathmini ya masuala mbalimbali ya haki za binadamu iliyofanyika kwa kutumia viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, kwa ujumla hali ya haki za binadamu nchini Tanzania kwa mwaka 2021 ilidorora kiasi ukilinganisha na mwaka wa 2020. Hali hiyo ilichangiwa zaidi na ukiukwaji wa haki za kiraia na kisiasa pamoja na haki za makundi maalum. Kama ilivyokuwa katika ripoti iliyopita, matukio mengi ya ukiukwaji wa haki za binadamu yalikuwa ni ya ukiukwaji wa haki za kiraia na kisiasa.

Mikoa ambayo masuala na aina nyingi za matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu yaliyoripotiwa ni pamoja na: Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Tanga, Katavi, Shinyanga, Mwanza, Morogoro, Mara, na Mbeya. Changamoto kuu zinazohusiana na haki za binadamu katika mikoa hii ni pamoja na ukatili wa kijinsia, ukatili dhidi ya watoto, ajira na utumikishwaji wa watoto, na ukiukwaji wa haki ya kuishi.

Masuala na aina nyingine za ukiukwaji wa haki za binadamu kwa upande wa Tanzania Bara kwa mwaka 2021 ni pamoja na ukiukwaji wa haki za wanahabri, mauaji yanayotokana na kujichukulia sheria mkononi, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, ukatili dhidi ya mwenza na mauaji yanayofanywa na mweza, usafirishaji haramu wa binadamu na watoto, utelekezaji wa watoto, ukeketaji, na ukiukwaji wa haki za kumiliki mali na urithi kwa upande wa wanawake (ikiwemo wajane).



02

SURA YA PILI:

# HAKI ZA KIRAIA NA KISIASA

# SURA YA PILI:
# HAKI ZA KIRAIA NA KISIASA

## Utangulizi

Sura hii inajadili hali ya haki za kiraia na kisiasa kwa mwaka 2021 upande wa Tanzania Bara, ikiangalia ukiukwaji wa haki hizo, masuala mbalimbali yaliyojitokeza, na mambo chanya yaliyofanyika. Sura hii imejikita katika Haki ya Kuishi, Uhuru wa Kujieleza, Haki ya Usawa mbele ya Sheria na Nafuu ya Kisheria, Haki ya kuwa Huru na Salama, Uhuru wa Kukusanyika, Uhuru wa Kujumuika, Uhuru dhidi ya Ukatili, Haki ya Kushiriki katika Utawala, na Uhuru dhidi ya Utesaji. Haki hizi zimelindwa katika mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu, ikiwemo Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) wa mwaka 1966 na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981.

**95%** **Zaidi ya 95% ya matukio ya wananchi kujichukulia sheria mkononi hutokea Tanzania Bara.**


Kwa mwaka 2021, hali ya haki za kiraia na kisiasa ilidorora kiasi ukilinganisha na mwaka 2020. Masuala mbalimbali yalichangia katika hili, hasa matukio ya ukiukwaji wa haki ya kuishi, sheria na kanuni zenye vifungu vinavyominya haki za binadamu, na vikwazo vya ufikiaji wa haki na haki jinai.

### 2.1. Haki ya Kuishi

Matukio mbalimbali kama vile mauaji yanayotokana na kujichukulia sheria mkononi, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, mauaji yanayotokana na na maafisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi, na mauaji yanayofanywa na mweza, yaliendelea kusababisha au kuhatarisha haki ya kuishi. Masuala mengine yaliyohatarisha na kukiuka haki ya kuishi ni pamoja na adhabu ya kifo na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino.


## *Mauaji yanayotokana naWananchi Kujichukulia Sheria Mkononi:*

Mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi yalisababisha vifo **239** katika kipindi cha Januari hadi Agosti 2021 pekee. Hadi kufikia mwezi Disemba 2021, idadi ya matukio hayo ilifikia **473,** sawa na ongezeko la asilimia **6.8** ukilinganisha na mwaka 2020.




*# Mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi, 2015 hadi 2020*
*Chanzo: Takwimu za Jeshi la Polisi*

Wanajamii wengi walioshiriki katika utafiti wa haki za binadamu walisema mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi ni tatizo kiasi **(49%)** na tatizo kubwa **(23%)** katika jamii zao. Kuhusu sababu za watu kujichukulia sheria mkononi, kutokuwa na imani na polisi **(57%)** kulitajwa kama sababu kuu. Sababu nyingine ni pamoja na haki kuonekana kuchukua muda mrefu kutendeka; mtuhumiwa kuonekana tena mtaani baada ya kukamatwa na polisi; kutokuwa na imani na mahakama; na uelewa mdogo kuhusu dhamana. LHRC ilikusanya matukio **22** ya mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi, ambayo ni idadi sawa na ile ya mwaka 2020. Matukio haya yaliripotiwa katika Mikoa ya Mwanza, Pwani, Rukwa, Lindi, Songwe, Katavi, Njombe, Morogoro, Manyara, Dodoma, Dar es Salaam, Shinyanga, na Tanga.




*%Majibu ya washiriki wa utafiti kuhusiana na sababu za wananchi kujichukulia sheria mkononi (N=1,092)*
*Chanzo: Taaarifa za utafiti, 2021*

***"Unajua bwana hawa wanaotuibia huku mtaani sio watu wa mbali, ni watoto wa humuhumu mtaani, tumekuwa nao. Kwa hiyo huwa tunajitahidi kuwa wastaarabu na kuwapeleka polisi, kwanza siku mbili tu unamuona mtaani, halafu kama haitoshi anaiba tena. Ukimfuata mzazi wake anakupa stori ndefu na kukataa mwanae sio mwizi. Akirudia tena, tunaamua tu kumalizana naye."***

**Mwananchi (ME), Dar es Salaam**

*"…..wezi wamezidi sana huku kijijini kwetu maana kila siku wakikamatwa na wakipelekwa polisi familia zao wanatoa rushwa wanaachiwa na kutamba mitaani. Kuna wezi wawili tumewachoma moto ili iwe fundisho kwa wengine….."*
**Mwananchi (KE), Pwani**

**Mtazamo & Wito wa LHRC:** Tatizo la wananchi kuamua kujichukulia sheria mkononi linaonekana kuchochewa zaidi na wao kutokuwa na imani na mfumo wa haki jinai. Katika muktadha huu, ni muhimu kufanya maboresho ya mfumo huu ili kurudisha imani ya wananchi. Lakini pia bado kuna haja ya wadau mbalimbali kuendelea kueneza uelewa kuhusu haki jinai na haki za mtuhumiwa ili kusaidia kuondoa baadhi ya mitazamo hasi miongoni mwa wanajamii.

Wananchi pia wanahimizwa kutojihusisha na vitendo vya mauaji yanayotokana na wao kujichukulia sheria mkononi na kuacha mkondo wa sheria ufanye kazi yake. Kadhalika, kuna haja ya kueneza uelewa kuhusu sheria na kanuni mbalimbali zinazohusiana na haki jinai, pamoja na madhara au athari zinazotokea sababu ya wananchi kujichukulia sheria mkononi.

### *Mauaji yanayotokana na maafisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi na ukatili unaofanywa dhidi ya maafisa wa vyombo hivyo*

Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya matukio tisa ya mauaji yanayotokana na maafisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi, mengi kati yao yakifanywa na askari Sungusungu, hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam. Matukio haya ni matukio matano zaidi ya yale yaliyoripotiwa na kukusanywa na LHRC mwaka 2020. Pia, LHRC ilikusanya matukio takribani manne ya ukatili unaofanywa dhidi ya maafisa wa vyombo vya dola, yakijumuisha askari polisi kuuwawa na mmoja kushambuliwa vibaya, ambayo yalitokea katika Mikoa ya Dar es Salaam na Arusha.

*"Kuna hao sungusungu ambao wameshahusika kwenye matukio ya kupiga watu hadi kupoteza maisha, hasa katika maeneo ya Mabibo, Magomeni, Tandale (Kwa Mtogole), na Manzese."*
**Mwananchi (KE), Dar es Salaam**


**Wito wa LHRC:** Maafisa wa vyombo vya dola, wakiwemo askari polisi, kutojihusisha na vitendo vya matumizi ya nguvu kupita kiasi na kinyume na sheria ambayo yanapelekea kutokea kwa vifo vya watuhumiwa wa uhalifu, ili kuendena na matakwa ya sheria/

viwango vya kitaifa na kimataifa, ikiwemo Mwongozo wa Utendaji Kazi katika Jeshi la Polisi/ Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi (PGO) na Kanuni za Umoja wa Mataifa za Utendaji Kazi wa Maafisa wa Vyombo vya Dola. Kuna haja pia ya kuundwa kwa chombo maalum cha kuchunguza utendaji kazi wa askari polisi, ambacho mojawapo ya kazi zake itakuwa ni kuchunguza tuhuma za mauaji yanayotokana na maafisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi.

**Wito wa LHRC:** Wananchi kutojihusisha na vitendo vya kuwashambulia maafisa wa vyombo vya dola, kwani kufanya hivyo siyo tu ni kosa kisheria, bali pia ni ukiukwaji wa haki za maafisa hao kama binadamu.

***Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino***

Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina yaliendelea kuathiri haki za binadamu mwaka 2021, hasa kwa upande wa wazee. Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Agosti 2021, Jeshi la Polisi lilirekodi jumla ya matukio 84 ya mauaji yanayotokana na imani za kishirikina. Hadi kufikia mwezi Disemba mwaka 2021, idadi ya matukio hayo ilifikia 155, sawa na ongezeko la matukio 43 (38.4%) ukilinganisha na mwaka 2020.




*#Matukio ya mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, 2015 hadi 2020*
*Chanzo: Takwimu za Jeshi la Polisi*

**Wazee ndiye wahanga wakubwa wa mauaji yanayotokana na imani za kishirikina.**

Kupitia ufuatiliaji wa haki za binadamu na utafiti wa taarifa zinazotolewa na vyombo vya habari, kwa mwaka 2021 LHRC ilikusanya matukio 36 ya mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, ambayo ni matukio 15 zaidi ya yale yaliyokusanywa mwaka 2020. Matukio hayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Dodoma, Kagera, Mbeya, Arusha, Katavi, Tabora, Songwe, Njombe, Kigoma, Rukwa, Manyara, na Shinyanga. Asilimia 55 ya wahanga walikuwa ni wanawake, wengi


wao wakiwa na umri wa miaka 50 na zaidi. Kwa upande wa mauaji ya watu wenye ualbino, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, hakukuwa na matukio yoyote ya mauaji yaliyoripotiwa, lakini hali ilibadilika mwaka 2021 baada ya kuripotiwa tukio moja la mauaji ya mtoto mwenye ualbino mkoani Tabora. Mtoto huyo, aliyekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 4 hadi 7, alikutwa akiwa ameuwawa kikatili na mwili wake kukatwakatwa wilayani Uyui. Pia, katika kipindi cha mwaka 2021, LHRC ilikusanya tukio moja la ufukuaji wa kaburi la mtu mwenye ualbino.

**Mtazamo wa LHRC:** Tukio la mauaji ya kikatili ya mtoto mwenye ualbino mkoani Tabora limerudisha nyuma juhudi zilizokuwa zimefanywa katika kuimarisha ulinzi wa watu wenye ualbino na kukotokomeza vitendo vya mauaji ya watu hao.

**Wito wa LHRC:** Kuna haja ya kufanya jitihada za pamoja upya kuimarisha ulinzi wa watu wenye ualbino nchini Tanzania. Juhudi hizi ziongozwe na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kama ilivyofanya kipindi cha nyumba, ikiwa ni pamoja na kuwaleta pamoja wadau mbalimbali wa kiserikali na wasio wa kiserikali ili kujadili na kuweka mikakati ya kupambana na vitendo vya ukatili na mauaji ambavyo watu wenye ualbino wanafanyiwa.

### *Adhabu ya kifo*

Japokuwa adhabu ya kifo imekuwa haitekelezwi katika vipindi vya marais watatu waliopita, adhabu hiyo imekuwa ikiendelea kutolewa na mahakama katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara. Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya matukio 24 ya adhabu ya kifo, ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Mara, Geita, Iringa, Njombe, na Kigoma. Matukio haya ni matukio 6 pungufu ya yale yaliyoripotiwa mwaka 2020.




*#Adhabu za kifo zilizokusanywa na LHRC – 2017 hadi 2021*
*Chanzo: LHRC, 2021*


**Mtazamo wa LHRC:** Adhabu ya kifo inakiuka haki ya kuishi na ni adhabu katili na isiyo ya kibinadamu kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa dhidi ya Utesaji. Tafiti mbalimbali zimeonyesha kwamba utoaji wa adhabu hii haujasaidia kupungua kwa uhalifu na ndiyo maana nchi nyingi duniani zimefanya na

zinaendelea kufanya maamuzi ya kuondoa adhabu ya kifo. Pia, kumekuwa na kesi mbalimbali duniani ambapo iligundulika kwamba mhanga wa adhabu ya kifo alikutwa na hatia na kuhukumiwa kimakosa, lakini tayari adhabu ilishatekelezwa na yeye kupoteza maisha kwa kosa ambalo hata hakulifanya.

**Wito wa LHRC:** Ikiwa ni miongoni mwa nchi ambazo hazitekelezi adhabu ya kifo, ipo haja ya Tanzania kujiunga na nchi nyingine nyingi duniani na kuchukua hatua ya kuondoa kabisa adhabu ya kifo. Kwa sasa, ni nchi 53 pekee ambazo zinaendelea kuwa na adhabu ya kifo na kutekeleza adhabu hiyo, huku nchi 29 zikiwa hazitekelezi adhabu hiyo, ikiwemo Tanzania. Nchi Jirani kama vile Rwanda na Msumbiji ni miongoni mwa nchi 106 duniani ambazo zimeondoa adhabu ya kifo, na Tanzania inaweza kupiga hatua zaidi na kuondoa adhabu hiyo. Mnamo mwezi Julai 2021, nchi ya Sierra Leone iliweka historia kwa kuwa nchi ya 110 kuondoa adhabu ya kifo kwa makosa yote duniani, baada ya Bunge la nchi hiyo kupitisha Sheria ya Kuondoa Adhabu ya Kifo ya mwaka 2021. Kwa kufanya hivyo, nchi hiyo inakuwa nchi ya pili kufanya hivyo mwaka 2021 baada ya Malawi kufanya hivyo mwezi Aprili 2021.

### *Ukatili dhidi ya mwenza na mauaji yanayofanywa na mwenza*

Kwa mwaka 2021, matukio ya ukatili dhidi ya mwenza na mauaji dhidi ya mweza yaliongezeka, ambapo wanawake ndiyo walikuwa wahanga wakubwa. LHRC ilikusanya jumla ya matukio 35 ya mauaji ya aina hii, ambayo yameongezeka kutoka matukio 32 yaliyoripotiwa na kukusanywa mwaka 2020. Matukio hayo yaliripotiwa katika mikoa 16 ya Tanzania Bara. Alisimia 89 ya wahanga walikuwa ni wanawake na alimia 72 ya matukio hayo ya mauaji yalisababishwa na wivu wa kimapenzi. Asilimia kubwa ya washiriki wa utafiti uliofanywa na LHRC katika mikoa 20 ya Tanzania Bara (37%) walisema kwamba ukatili dhidi ya mwenza na mauaji yanayofanywa na mwenza yanayosababishwa na wivu wa kimapenzi ni tatizo kiasi katika jamii zao




*Wahanga wanawake wa mauaji yanayofanywa na mwenza*

*"Hapa kwetu Masasi kuna matukio matatu ya wanawake kubakwa na wapenzi wao na kuwauwa na wanaume kukimbia kusipojulikana kwa kipindi cha mwaka 2020/2021 na kesi zipo hadi sasa mahakamani"*
**Mwanajamii (ME), Masasi – Mtwara**

*"…wivu wa mapenzi ni chanzo kikubwa cha mauaji ya wenza…wakurya wana wivu sana kwa wapenzi wao na ikitokea akamhisi mke wake anachepuka kumpiga hadi kumuua ni jambo la kawaida tu.."*
**Mwanajamii (ME), Mara**

**Mtazamo wa LHRC:** Tangu mwaka 2019, kesi za wanawake kuuwawa na wenza wao zimekuwa zikiongezeka na kuna wasiwasi kwamba kuna matukio mengine mengi ya aina hiyo ambayo hayaripotiwi au kurekodiwa kama aina hiyo ya mauaji. Kuongezeka kwa mauaji haya kunahatarisha haki mbalimbali za wanawake, ikiwemo haki ya kuishi, haki ya afya, na haki ya kuwa salama. Hali hii inathibitisha matokeo ya utafiti kuhusu mauaji ya wanawake uliofanywa na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Madawa na Uhalifu (UNODC) mwaka 2018, ambayo yalionyesha kwamba nyumbani ndiyo mahala hatari zaidi kwa wanawake, sababu ya kuuwawa na wenza au wanafamilia.

**Wito wa LHRC:** Kuna haja ya wadau wote kuunganisha nguvu na kutengeneza mikakati ya kuwalinda wanawake dhidi ya ukatili dhidi ya mwenza na/au ukatili majumbani, kwa kuwa ndiyo wamekuwa wahanga zaidi. Sehemu nzuri ya kuanzia ni utungaji wa sheria ya ukatili wa kijinsia au ukatili majumbani ili kuwalinda wenza, kwa kuwa imeshafahamika kwamba matukio mengi ya ukatili wa kijinsia hutokea nyumbani. Mkakati mwingine unaweza kuwa kufanya kampeni kubwa ya kueneza uelewa kuhusu ukatili dhidi ya mwenza na madhara ya ukatili huo katika ngazi mbalimbali, ikiwemo mtu binafasi, familia, jamii, na taifa.

### *Matukio ya watu kupotea*


Matukio ya watu kupotea yalileta pia changamoto kwenye haki ya kuishi mwaka 2021. Katika mwaka huo, LHRC ilikusanya matukio ya kupotea takribani watu 12, ambao walidaiwa kuchukuliwa na watu wasiojulikana na kupotea. Matukio hayo yaliripotiwa katika mikoa ya LIndi na Dar es Salaam, na wahanga wote walikuwa ni wanaume. Kuna matukio kadhaa ya watu kupotea pia bado hayajapatiwa majibu, ikiwemo kupotea kwa Azory Gwanda, Ben Saanane, na Simon Kanguye.

**Mtazamo wa LHRC:** Matukio ya watu kupotea na kutokuwepo kwa taarifa za mara kwa mara kuhusiana na mahala uchunguzi ulipofikia na nini kinaweza kuwa kiliwakumba watu hao kunakiuka wajibu wa Serikali katika mikataba mbalimbali ya haki za binadamu wa kufanya uchunguzi wa kina pale ambapo watu wameuwawa au 'kupotea/kupotezwa.'

**Wito wa LHRC:** Serikali na Jeshi la Polisi Tanzania kuongeza kasi ya chunguzi za kupotea kwa Azory Gwanda, Ben Saanane na watu wengine na kutoa mrejesho mara kwa mara. Kufanya hivi kutazisaidia familia za watu hao waliopotea kupata amani ya moyo na pale ambapo waliowateka ndugu zao wamepatikana, basi sheria ifuate mkondo wake. Pia, tunapenda kumshauri Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pale itakapoonekana ni sahihi, kuunda tume ya uchunguzi wa upoteaji wa watu na hata kuomba msaada kutoka vyombo vya nchi nyingine kusaidia katika uchunguzi.

### *Ajali za barabarani*


Kwa mwaka 2021, ajali za barabarani na vifo vinavyotokana na ajali hizo vilipungua, kwa kiasi kikubwa kwa sababu ya juhudi za Jeshi la Polisi. Ajali hizo zilipungua kutoka 10,297 mwaka 2016 hadi 2,924 mwaka 2019. Kwa mwaka 2020, Jeshi la Polisi Tanzania lilipoti kutokea ajali za barabarani 1,933, ambazo zilisababisha vifo 1,384, wakati kwa mwaka 2021, idadi ya ajali za barabarani ilipungua zaidi hadi kufikia 1,864 (sawa na punguzo la aslimia 3.6) na vifo pia vilipungua kufikia 1,368 (sawa na punguzo la asilimia 1.2).




*#Ajali za barabarani na vifo nchiniTanzania, 2015 hadi 2021*

Ajali nyingi za barabarani (asilimia 91.6) zinasababishwa na makosa ya kibinadamu, na kati ya ajali hizo zinazosababishwa na makosa ya kibinadamu, mengi (asilimia 34.89), yanasababishwa na uzembe wa dereva, ukifuatiwa na uzembe wa madereva bodaboda (asiimia 17.91%) na kuendesha chombo cha usafiri kwa kasi kupita kiasi (asilimia 15.87) .

Sababu za Ajali ya Barabarani- 2020




*%Vyanzo vya ajali za barabarani Tanzania Bara, 2020*

*Chanzo: Takwimu za Polisi na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2020*

**Mtazamo wa LHRC:** Japokuwa idadi ya ajali za barabarani na vifo vinavyotokana na ajali hizo vimepungua tangu mwaka 2016, idadi ya vifo bado iko juu na vifo hivyo vimeleta madhara makubwa katika jamii na uchumi wa nchi. Madereva wa malori na mabasi yanayosafiri kuelekea maeneno mbalimbali ya Tanzania Bara wamekuwa wakilalamikiwa kusababisha ajali za barabarani. Hili linachangiwa na wao kufanyishwa kazi kupita muda maalum uliobainishwa katika sheria na kanuni za kazi na kupewa muda mfupi wa kukamilisha kazi, hivyo kusababisha kukosa muda wa kutosha wa kupumzika, jambo ambalo linachangia ajali za barabarani.

**Wito wa LHRC:** Jeshi la Polisi na wadau wengine, wakiwemo wakala wa barabara, kuongeza juhudi za kuhakikisha usalama barabarani na kuzuia ajali za barabarani. Pia, kuna haja ya kuongeza usimamizi na utekelezaji wa sheria za usalama barabarani, ikiwemo Sheria ya Usalama Barabarani. Tunatoa rai pia kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri, hasa mabasi na malori, kuhakikisha madereva wao hawafanyi kazi kupita muda uliowekwa kisheria na wanazingatia sheria na kanuni za usalama barabarani, ili kuzuia na kupunguza ajali hizo. Tunawaasa pia wananchi kuzingatia sheria na kanuni za usalama wa barabarani na kujiepusha na vitendo vyote vinavyoweza kupelekea kutokea kwa ajali, kama vile kuendesha vyombo vya usafiri wakiwa wamelewa, kuendesha kwa kasi kupita kiasi, kuvipita vyombo vya usafiri vingine barabarani bila kuchukua tahadhari, na kutofunga mkanda kwenye gari.

## 2.2. Uhuru wa Kujieleza

Hali ya uhuru wa kujieleza, hususan uhuru wa vyombo vya Habari, haikubadilika sana mwaka 2021 ukilinganisha na mwaka 2020, ambapo Tanzania iliendelea kushikilia nafasi ya 124 katika viwango vya uhuru wa habari duniani vya mwaka 2021. Masuala makuu kuhusiana na uhuru wa vyombo vya habari

kwa mwaka 2021 ni pamoja na sheria na kanuni zenye vifungu vinavyominya uhuru huo, ambavyo vinakinzana na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu; ukamataji na uwekaji kuzuizini kinyume na sheria; vitisho; na upatikanaji wa taarifa. Sheria ambazo zina vifungu vinavyominya uhuru wa vyombo vya habari kinyume na viwango vya kimataifa vya uhuru huo ni pamoja na Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016, Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015, na Kanuni za Maudhui ya Mtandao za mwaka 2020. Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya jumla ya matukio saba ya ukamataji na uwekaji kizuizini kinyume na sheria wa wanahabari, ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kilimanjaro, na Katavi.

Wanahabari ambao walishiriki katika ufafiti kuhusu haki za binadamu uliofanywa na LHRC mwaka 2021 waliibua changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo katika kufanya kazi zao, ikiwemo uelewa mdogo kuhusu sheria na kanuni, ambapo LHRC iligundua kwamba nusu ya washiriki hawakuweza kutaja kwa usahihi walau sheria tatu za habari. Nusu ya washiriki pia walizitaja sheria zenye vifungu vinavyominya uhuru wa vyombo vya habari kama tatizo kubwa katika mazingira yao ya kazi, huku asilimia 48 wakitaja vifaa vyao kuchukuliwa au kuharibiwa kama tatizo kiasi. Haki kuu tatu za wanahabari ambazo zilitajwa kukiukwa zaidi ni uhuru wa vyombo vya habari (77%), haki ya kupata taarifa (68%) na uhuru wa kutoa maoni (64%).

Ukiacha changamoto mbalimbali zilizojitokea katika sekta ya habari mwaka 2021, Mh. Rais Samia Saluhu Hassan alitoa maagizo kwa mamlaka za serikali kuvifungulia vyombo mbalimbali vya habari ambavyo vilikuwa vimefungiwa katika mwaka/miaka iliyopita. Pia, mwaka 2021 kulikuwa na marekebisho chanya ya Kanuni za Maudhui ya Mtandao za mwaka 2020, na Kanuni za Televisheni na Redio, japokuwa kwa upande wa Kanuni za Maudhui ya Mtandao za mwaka 2020 bado kuna vifungu vingi vinavyominya/kuhatarisha uhuru wa kujieleza, ambavyo na vyenyewe vinatakiwa kufanyiwa marekebisho ili kuendana na viwango vya kimataifa vya uhuru wa kujieleza.

## 2.3. Uhuru wa Kujumuika na Kukusanyika

Sheria kadhaa ziliendelea kuwa mwiba kwa uhuru wa kujumuika na kukusanyika mwaka 2021 kwa kuwa na vifungu vinavyominya uhuru huo, kinyume na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Vyama vya kisiasa, ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka

2019, na Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu wa Msingi (BRADEA), ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2020. Kwa sababu hizi, pamoja na katazo la kufanya mikutano ya hadhara ya kisiasa nje ya jimbo, lilitolewa mwaka 2016 na ambalo bado halijaondelewa rasmi, zimechangia katika kudorora kiasi kwa uhuru wa kujumuika na kukusanyika kwa mwaka 2021.

Kwa mwaka 2021, LHRC pia ilikusanya matukio matatu ya ukiukwaji wa uhuru wa kujumuika na kukusanyika wa vyama vya kisiasa, yote yakikihusisha chama kuu cha upinzani, CHADEMA. Matukio hayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, na Mara.

## 2.4. Haki za Usawa mbele ya Sheria na Nafuu ya Kisheria

Pamoja na juhudi na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali na Mhimili wa Mahakama kukuza na kulinda haki za usawa mbele ya sheria na nafuu ya kisheria, bado kuna changamoto kadhaa zinazozuia utekelezaji madhubuti wa haki hizi. Kwa mwaka 2021, masuala muhimu yaliyoathiri haki za usawa mbele ya sheria na nafuu ya kisheria ni pamoja na: sheria zinazoathiri utekelezaji madhubuti wa haki ya usawa mbele ya sheria; vikwazo vya ufikiaji wa haki, ikiwemo upungufu wa watumishi/wafanyakazi wa kimahakama, ucheleweshaji katika chunguzi, na urefu wa kesi; na changamoto za haki jinai kama vile uwekaji kuzuizini wa mahabusu magerezani kwa muda mrefu, chunguzi kuchukua muda mrefu na kesi kuahirishwa mara kwa mara, msongamano wa mahabusu magerezani na katika vituo vya polisi, changamoto za utaratibu wa kikiri kosa, mtuhumiwa kutofikishwa mahamani ndani ya muda unaotakiwa kisheria, haki za wafungwa na mahabusu, makosa yasiyo na dhamana, na matumizi ya video katika mashauri ama kesi za jinai.

Marekebisho ya Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu wa Msingi (BRADEA) ya mwezi Juni mwaka 2020 yalikosolewa ndani na nje ya nchi kwa kukinzana na kukiuka viwango vya kimataifa vya haki za binadamu. Athari ya marekebisho hayo iliendelea kuonekana mwaka 2021, hasa katika kwa upande wa ufikiaji wa haki, ambapo asasi za kiraia ziliendelea kushindwa kufungua kesi kwa niaba ya wahanga wa ukiukwaji wa haki za binadamu, hivyo kuathiri nafasi yao ya kukuza na kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu.

***Kuhusiana na ufikiaji wa haki***, kwa mwaka 2021 Serikali na Mhimili wa Mahakama

uliendelea kuchukua hatua mbalimbali kuimarisha ufikiaji wa haki, ikiwemo ujenzi na ukarabati wa majengo ya mahakama, uteuzi wa Majaji wapya wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani, matumizi ya TEHAMA kuboresha ufikiaji au upatikanaji wa haki, na utekelezaji na mapendekezo ya upanuzi wa programu ya mahakama zinazotembea.


Mwezi Februari mwaka 2021, Bunge la Tanzania lilipitisha muswada wa marekebisho ya sheria kuifanya Lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya mahakama na sheria, ambao ulisainiwa na Rais na kuwa sheria mwezi Aprili 2021. Wanajamii na wanasheria mbalimbali walioshiriki katika utafiti walikuwa na maoni tofauti kuhusu maamuzi haya ya Serikali.

*"Kwa maoni yangu naona isibadilishwe, ibaki ya Kiingereza maana Kiswahili kina misamiati migumu. Pia, changamoto kubwa ni kupata maneno sahihi yenye kuleta maana nzuri."*
**Mwanasheria, Mara**

*"Ni hatua chanya kwani itapelekea Watanzania walio wengi kuelewa na kuzitambua sheria ili kurahisisha matumizi yake katika shughuli zao na katika upatikanaji wa haki."*
**Hakimu Mkazi, Mwanza**

***Wanajamii walioshiriki katika utafiti wa haki za binadamu mwaka 2021 walitambua vikwazo kadhaa vya ufikiaji wa haki.***

Rushwa ilitajwa kama kikwazo kikubwa kuliko vyote (asilimia 79), ikifuatiwa na urefu wa kesi au mashauri mahakamani (asilimia 48), uelewa mdogo kuhusu sheria miongoni mwa raia (asilimia 47), na gharama za uwakilishi mahakamani (asilimia 37). Vikwazo vingine vilivyotajwa na robo wa washiriki ni pamoja na taratibu ndefu na ngumu za kisheria na lugha ya mahakama na sheria. Takribani theluthi mbili ya washiriki (asilimia 62) walisema upungufu wa watumishi wa mahakama ni kikwazo cha ufikiaji wa haki katika jamii zao. Kwa sasa, Mhimili wa Mahakama unakabiliwa na upungufu wa watumishi 4,728 (sawa na asilimia 46), jambo ambalo limeathiri utoaji wa haki. Hali kadhalika, pamoja na juhudi mbalimbali za wadau, ikiwemo wasaidizi wa kisheria, bado kuna changamoto katika ufikiaji na upatikanaji wa haki, hasa kwa maeno ya vijijini na pembezoni. Suala hili lilitajwa kama kikwazo cha ufikiaji haki na asilimia 23 ya washiriki.




*%Vikwazo vya ufikiaji haki*

*"Vijijini kuna rushwa sana...mfano huko kijijini mtu lazima atoe Tsh. 100,000/= ili afungue kesi. Hili ni tatizo zaidi katika mahakama za mwanzo na za wilaya…"*
**Afisa shirika la kijamii, Geita**

Baadhi ya washiriki wa utafiti wa haki za binadamu, hasa mawakili, walisema kwamba rushwa katika mahakama za chini, Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya, inachangiwa na mazingira yasiyoridhishwa ya ufanyaji kazi kwa mahakimu, ikiwemo mishahara midogo na kutolipwa fedha za kujikimu.

### *Changamoto za Haki Jinai*

Kwa upande wa haki jinai, uwekaji kuzuizini wa muda mrefu ulitajwa kama changamoto kubwa zaidi kwa mahabusu. Mwezi Agosti 2021, Mh. Rais Samia Suluhu Hassan alisema kwamba uwekaji wa mahabusu kuzuizini kwa muda mrefu siyo tu unaleta mzigo kwa Serikali, bali pia ni ukiukwaji wa haki zao za msingi. Washiriki wengi wa Utafiti wa Haki za Binadamu wa mwaka 2021, ikiwemo wanajamii, wanasheria, na maafisa wa mashirika yasiyo ya kiserikali, walisema kwamba uwekaji kizuizini wa mahabusu kwa muda mrefu ni changamoto kubwa nchini Tanzania, hali inayochangia msongamano magerezani na ukiukwaji wa haki za msingi za watuhumiwa. Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Disemba 2021, LHRC ilikusanya kesi 11 za watu waliopo magerezani kwa muda unaofikia miaka 6 hadi 12 wakisuburia kesi kuanza kusikilizwa. Pia, kupitia mitandao ya kijamii, LHRC ilifuatilia na kukusanya kesi nyingine nane za uwekaji kuzuizini wa mahabusu wa muda mrefu.

**19** **kesi za uwekaji kuzuizini kwa muda mrefu zilizokusanywa na LHRC mwaka 2021.**

*"Jela nyingi zimejaa sio kwa sababu wafungwa ni wengi ila ni kwasababu mahabusu wanachanganywa na wafungwa yaani wanakua 'treated' kama wafungwa. Watuhumiwa wengi wanakamatwa na*

***kufungwa ili kupisha upelelezi uendelee badala ya kukamilisha kwanza upelelezi ndipo mtuhumiwa akamatwe. Pili, kuna makosa madogo ambayo mtu angeweza kukamatwa na kushitakiwa hata kifungo cha nje lakini badala yake makosa mengi wote hufungwa gerezani. Hili hii inafanya kuwe na idadi kubwa ya wafungwa na magereza kuzidiwa."***

**Wakili, Morogoro**


> Watu maskini na walio pembezoni, wakiwemo wanawake na watoto, wanaathiriwa zaidi na uwekaji kizuizini kwa muda mrefu wa mahabusu.

Uwekaji kizuizini wa watuhumiwa/ mahabasu kwa muda mrefu unapunguza nafasi ya haki ya kesi kuendeshwa kwa haki na dhana ya mtuhumiwa kutochukuliwa mwenye hatia hadi pale ambapo mahakama itasema vinginevyo. Pia, changamoto hii inawafanya mahabusu kuwa katika hatari kubwa zaidi ya kufanyiwa vitendo vya utesaji na kutokuwa na uwakilishi mzuri mahakamani, hasa pale ambapo mahabusu hao ni watu maskini. Pia kuna madhara ya kiuchumi na kijamii yanayotokana na uwekaji kuzuizini wa muda mrefu wa mahabusu, ikiwemo kupoteza mtafuta mkate wa familia, kuvunjika au kuvurugika kwa familia, kupoteza makazi au sehemu ya kuishi, kupoteza michango ya hifadhi ya jamii, kukatisha masomo, unyanyapaa, msongo wa mawazo, na kutoajiriwa ua kutopata ajira stahiki kwa muda mrefu. Kwa upande wa jamii na taifa, athari ni pamoja na kudhoofisha utawala wa sheria, kutengeneza mazingira ya rushwa, kupoteza vipaji, msongamano katika magereza, na kupoteza imani na mfumo wa haki.

Changamoto nyingine katika haki jinai ni pamoja na: ucheleweshaji katika chunguzi na uahirishaji wa mara kwa mara wa kesi; msongamano magerezani/mahabusu; ulinzi wa haki za mtuhumiwa katika utaratibu wa kukiri kosa; ucheleweshaji katika kufikisha watuhumiwa mahakamani; ukiukwaji wa haki za wafungwa na mahabusu; kukosekana kwa utaratibu mzuri na rasilimali za kutosha kwa ajili ya kuwasaidia wafungwa au mahabusu waliotoka magerezani kurudi katika jamii, ikiwemo msaada wa kisaikolojia; na kutotolewa dhamana kwa makosa yasiyo na dhamana. Kwa sasa, asilimia 53 ya watu walio magerezani ni mahabusu.

***"...Wafungwa na mahabusu hawafurahii haki zao za msingi kama vile haki ya faragha na wenza wao, kupata chakula kizuri, afya, mazingira bora ya kuishi na haki ya kutotendewa vitendo vya ukatili."***

**Wakili, Dar es Salaam**




Kwa ujumla, washiriki wa utafiti walikuwa na maoni tofauti kuhusu **utaratibu wa kisheria wa kukiri kosa** na utekelezaji wake mpaka sasa, wengi wao, hasa wanasheria, wakiupinga. Wasiwasi wao mkubwa kuhusiana na utaratibu huo wa kisheria katika haki jinai ni pamoja na uwezekano mkubwa wa mtuhumiwa kushurutishwa kukiri kosa; matumizi mabaya ya madaraka kutokana na mwendesha mashtaka kupewa mamlaka makubwa; kupunguza nafasi na mamlaka ya mahakimu na majaji kutika utoaji haki; na hatari ya watuhumiwa kuamua kukiri makosa ambayo hawajayafanya ili tu wapate kuwa huru tena.

**Wito wa LHRC:** Serikali kuhakikisha inachukua hatua kupunguza uwekaji wa watuhumiwa kuzuizini. Ni vizuri utaratibu huu ukatumika pale ambapo hakuna namna nyingine ya kuhakikisha mtuhumiwa hatoroki au kutofika mahakani atakapohitajika.

## 2.5. Haki ya kuwa Huru na Salama

Katika kipindi cha Januari hadi Disemba mwaka 2021, haki ya kuwa huru na salama iliathiriwa zaidi na ukamataji na uwekaji kizuizini kinyume na sheria; kunyimwa dhamana; kubambikiwa kesi; kukosekana kwa vituo vya polisi katika baadhi ya kata; wasiwasi kuhusiana na usalama na ulinzi wa watoto na wanawake, hasa kwa sababu ya vitendo vya ukatili; ucheleweshaji katika kufanya na kukamilisha chunguzi; na usafarishaji haramu wa binadamu.

***Kukosekana kwa vituo vya polisi*** katika baadhi ya kata kulichangiwa na mianya katika mipango ya maendeleo na upungufu wa askari polisi. Kwa mfano, wakati kiwango kinachotakiwa cha uwiano wa askari polisi na raia ni askari polisi mmoja kwa raia 450 ( 1:450), kwa sasa kuna askari polisi mmoja kwa raia 2,000 (1:2,000). Kufikia mwezi Disemba 2020, mikoa ambayo ilikuwa inaongoza kwa kuwa na upungufu wa askari polisi ni Simiyu (1:3,465), Tabora (1:2,768); Geita (1:2,457), Songwe (1,2,417), na Kigoma (1:2,342).


Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya jumla ya matukio nane ya kushambuliwa na kuuwawa

kwa madereva bodaboda, ambayo ni matukio matatu zaidi ya yale yaliyoripotiwa na kukusanywa mwaka 2020. Matukio hayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Dar es Salaam, Mara, Mbeya, Lindi, Pwani, na Tabora.

***Kuhusiana na ukamataji kinyume na sheria*** kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya takribani matukio nane, ikiwemo matano yanayowahusu wanahabari, sawa na ongezeko la tukio moja ukilinganisha na mwaka 2020.

***Kuhusiana na dhamana***, washiriki wengi wa utafiti wa haki za binadamu (asilimia 46) walisema kwamba kunyimwa dhamana ni tatizo kiasi, wakifuatiwa na wale waliodai kwamba ni tatizo kubwa (asilimia 35). Wanajamii pia walikuwa na maoni tofauti kuhusu pendekezo la makosa yote kutolewa dhamana.

Wanajamii wengi walioshiriki katika ufatifi (asilimia 49) walisema pia kwamba umbambikaji wa kesi ni tatizo kubwa katika jamii zao, wakifuatiwa na waliosema ni tatizo kiasi (asilimia 38). Ikumbukwe kwamba mwaka 2021 Mh. Rais Samia Suluhu Hassan pia alielezea wasiwasi wake kuhusiana na changamoto kadhaa katika haki jinai, ikiwemo ubambikaji wa kesi. Mnamo mwezi Mei mwaka 2021, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilitangaza kufuta kesi 147 ambazo zilionekana kuwa ni za kubambika. Mwaka 2021, LHRC pia ilikusanya matukio matatu ya ubambikaji kesi/makosa, ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Arusha na Tabora.




*%Mitazamo ya wanajamii kuhusu ubambakaji wa kesi/makosa (N=1,089)*

***Usafirishaji haramu wa binadamu ni tishio kwa haki ya kuwa huru na salama pamoja na haki nyingine kama vile haki ya kuishi,*** haki ya kutobaguliwa, uhuru dhidi ya utumwa, uhuru dhidi ya utesaji, uhuru dhidi ya ukatili, uhuru wa kujumuika, uhuru wa mtu kwenda atakako, haki ya afya, haki ya mazingira bora ya kazi, haki ya kuishi katika hali inayofaa, na haki ya hifadhi ya jamii. Kwa mwaka 2021, janga la Uviko19 liliongeza hatari ya watu kuwa wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu sehemu

mbalimbali duniani.

Takwimu za hivi karibuni za Jeshi la Polisi zinaonyesha kwamba jumla ya matukio 151 ya usafirishaji haramu wa binadamu yaliripotiwa katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2020. Kati ya matukio haya, matukio 19 yaliripotiwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la tukio moja ukilinganisha na mwaka 2019. Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya takribani matukio 20 ya usafirishaji haramu wa binadamu, ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Mara, Dodoma, Mbeya, Shinyanga, na Geita. Pia, iliripotiwa kwamba jumla ya Watanzania 163 waliokolewa na wadau wa kiserikali na wasio wa kiserikali kutoka katika biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu katika kipindi cha mwezi Julai 2020 na Machi 2021. Miongoni mwa watu hao ni watu wawili ambao waliokolewa katika nchi za Iraq na Malaysia.

Asilimia 97 ya biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu hufanyika ndani ya Tanzania, ambapo watoto wenye umri kati ya miaka 12 hadi 17 wamesemekana kuwa wahanga wakubwa. Wanawake na wasichana pia walitajwa kuwa wahanga wakubwa wa usafirishaji haramu wa binadamu. Usafirishaji haramu wa watoto, hasa kwa ajili ya kufanya kazi na kutumikishwa kingono, pia ni tatizo ambalo linakua siku hadi siku, huku asilimia 74 ya wahanga wakiwa ni wasichana. Mikoa ambayo inaongoza kwa usafirishaji haramu wa binadamu ni pamoja na Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Kigoma, Kagera, Geita, Singida, Arusha, Manyara, Shinyanga, Simiyu, Lindi, na Mtwara.

Usafirishaji haramu wa watu wenye ulemavu pia umekuwa tatizo kubwa. Mnamo mwezi Julai mwaka 2021, watu 15, ikiwemo mfanyabiashara mmoja, walikamatwa jijini Dar es Salaam kwa tuhuma za kuwasafirisha kiharamu watu 37 wenye ulemavu, wakiwemo watoto wenye ulemavu wenye umri wa miaka kati ya 7 na 11, kutoka katika Mikoa ya Tabora na Shinyanga na kuwapeleka jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kuomba na kuwapatia wao kipato.

## 2.6. Haki ya Kushiriki katika Utawala

Haki ya kushiriki katika utawala pia inafahamika kama haki ya kushiriki katika masuala ya umma au haki ya kushiriki katika serikali. Haki hii inajumuisha haki ya kupiga kura na kugombea nafasi za uongozi na haki ya kushiriki katika siasa. Katika kipindi cha miaka mingi huko nyuma, Serikali imechukua hatua kadhaa za kisheria na kitaasisi kuongeza na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika siasa. Hata hivyo, bado kuna vikwazo kadhaa ambavyo vinazuia

utekelezaji madhubuti wa haki za kugombea nafasi za uongozi na kushiriki katika siasa. Vikwazo hivi vimeonekana katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na sheria za uchaguzi, ikiwemo Sheria ya Vyama vya Siasa iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019. Kwa mfano, Katiba haitambui wagombea binafsi, na inakataza matokeo ya urais kuhojiwa au kupingwa mahakamani. Marekebisho yaliyofanywa kwenye Sheria ya Vyama vya Siasa yameathiri zaidi haki ya kushiriki katika siasa, hasa kwa kumpatia Msajili wa Vyama vya Siasa mamlaka makubwa ambayo yanaingilia uhuru wa vyama vya siasa. Kwa upande wa wanawake, ushiriki usioridhisha katika siasa na uongozi unachangiwa kwa kiasi na sheria ambazo hazijazingatia masuala ya usawa wa kijinsia, jambo linalofanya washindwe kushiriki kikamilifu katika siasa na kuwa na uwakilishi mzuri katika nafasi mbalimbali za uongozi.

Wakati nchi ikielekea katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, kuna masuala kadhaa ya kujifunza kutoka kwa nchi jirani ya Malawi, hususan uchaguzi wa urais wa mwaka 2019 na uchaguzi wa marudio wa urais wa mwaka 2020. Masuala haya ni pamoja na uhuru na nafasi ya Mhimili wa Mahakama katika kulinda haki wakati wa uchaguzi; matokeo ya urais kuweza kupingwa mahakamni; na uhuru na uadilifu wa vyombo vya usimamizi wa uchaguzi.

## 2.7. Uhuru dhidi ya Utesaji na Kutendewa kama siyo Binadamu

Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya takribani matukio 47 ya utesaji na/au kutendewa kama siyo binadamu. Matukio haya ni pamoja na watuhumiwa kuteswa wakati wapo chini ya ulinzi wa polisi na utesaji wa watoto, hasa majumbani. Matukio ya utesaji wakati watuhumiwa wapo chini ya ulinzi wa polisi yaliripotiwa katika Mika ya Mara, Dodoma, na Dar es Salaam.

## 2.8. Uhuru dhidi ya Ukatili

Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya matukio ya aina mbalimbali za ukatili ambao walifanyiwa wanawake, watoto, wanaume, watu wenye ulemavu, na wazee, ambayo yalipelekea ukiukwaji wa haki yao ya uhuru dhidi ya ukatili. Kuhusiana na ukatili dhidi ya wanaume, washiriki wengi wa utafiti wa haki za binadamu (asilimia 71) walisema kwamba aina hii ya ukatili siyo tatizo katika jamii zao, huku robo ya washiriki wakisema ni tatizo kiasi na asilimia 4 wakisema ni tatizo kubwa. Matukio ya ukatili dhidi ya wanaume yaliripotiwa zaidi katika Mikoa ya es Salaam, Songwe, Mara, na Shinyanga. Matukio hayo ni pamoja na kuuwawa kwa wanaume wanne katika mikoa hiyo, ambao waliuwawa na wenza wao, huku watatu kati yao wakiuwawa sababu ya wivu wa kimapenzi.

## 2.9. Athari ya Uviko19 kwa Haki za Kiraia na Kisiasa

Kwa mwaka 2021, athari ya Uviko19 katika haki za kiraia na kisiasa ilikuwa kubwa. Haki hizo ziliathiriwa kwa namna mbalimbali, ikiwemo:

- Wanahabari kushindwa kutembelea maeneo mbalimbali kutafuta taarifa
- Ucheleweshaji katika utoaji haki sababu ya changamoto za TEHAMA kama vile mtandao intaneti kuwa chini, baada ya Mhimili wa Mahakama kuamua kutumia teknolojia ya video kuendesha kesi ili kukabiliana na changamoto ya Uviko19

***"Washtakiwa hawaletwi mahakamani hasa kesi za kutajwa, tunawasomea kwenye video. Unakuta network mbovu, sauti inakata kata, mshtakiwa hatumsikii tunalipeleka tu so haki ya kusikilizwa ni ishu."***
**Afisa wa mahakama, Mwanza**

- Uahirishaji wa kesi wa mara kwa mara, ambao unaongeza ukubwa wa tatizo la uwekaji kuzuizini kwa muda mrefu kabla ya kesi kuanza kusikilizwa
- Mtuhumiwa kukosa haki yake ya kuwepo mahakamani
- Kubanwa zaidi kwa uhuru wa vyombo vya habari
- Kuongezeka kwa vitendo vya ukatili, hasa ukatili dhidi ya watoto na wanawake
- Vyombo vya habari kukabiliwa na changamoto ya kifedha na kulazimika kupunguza wafanyakazi, jambo ambalo liliathiri ukusanyaji na usambazaji wa habari
- Makundi kama watoto na wanawake kuwa katika hatari zaidi ya usafirishaji haramu wa binadamu
- Kuongezeka kwa ajira za watoto na utumikishwaji kiuchumi wa watoto



03

SURA YA TATU:

# HAKI ZA KIUCHUMI, KIJAMII NA KIUTAMADUNI

SURA YA TATU:

# HAKI ZA KIUCHUMI, KIJAMII NA KIUTAMADUNI

## Utangulizi

Kwa mwaka 2021, hali ya haki za kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni ilidorora kiasi, huku janga la Uviko19 likichangia hali hiyo. Changamoto mbalimbali ziliendelea kuathiri utekelezaji madhubuti wa haki hizo, ikiwemo ufinyu wa bajeti; ucheleweshaji wa fedha; kutotolewa kwa kiasi chote cha fedha za bajeti; mazingira yasiyoridhisha ya kazi; ukosefu wa ajira; upungufu wa wafanyakazi; na upungufu wa vifaa, nyenzo na majengo.

## 3.1. Haki ya Elimu

Wakati Serikali ikichukua hatua mbalimbali kuhakikisha utekelezaji wa haki ya elimu kulingana na rasilimali zilizopo, ikiwemo kupitia utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo ya ada, changamoto kadhaa ziliendelea kuathiri utekelezaji madhubuti wa haki hiyo mwaka 2021. Changamoto hizi ni pamoja na: wasiwasi kuhusiana na ubora wa elimu, ambao ulichangiwa na mazingira yasiyoridhisha ya kufundishia na kusoma; mianya katika mitaala; lugha ya kufundishia; upungufu wa walimu, ikiwemo walimu wa sayansi na elimu maalum; ufinyu wa bajeti; upungufu wa madarasa, madawati, na matundu ya vyoo; umbali mrefu kutoka nyumbani hadi shule; upatikanaji wa taulo za kike; baadhi ya wazazi kutokuwa tayari kuwapeleka watoto shule; kuacha shule; ukatili dhidi ya watoto wa shule, hasa ukatili wa kingono; na ndoa na mimba za utotoni.

Mianya katika utoaji wa elimu ya afya ya uzazi ilitajwa pia kama changamoto katika utekelezaji wa haki ya elimu. Baadhi ya vikwazo vikubwa katika utoaji wa elimu hiyo ni pamoja na kutokuwepo kwa fedha za kutosha kwa ajili ya utoaji wa elimu, baadhi ya mada muhimu kuondolewa au kutofundishwa, na kutokuwepo kwa

mafunzo ya kutosha na msaada kwa walimu. Vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, hasa ukatili wa kingono (ubakaji na ulawiti), viliendelea kuwa changamoto kwa watoto waliopo shule, hasa wasichana, na kuathiri ufurahiaji na utekelezaji wa haki yao ya elimu. Walimu wa kiume walitajwa kuwa miongoni mwa watu wanaofanya vitendo vya ukatili wa kingono dhidi ya wasichana shuleni. Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya matukio 10 ya walimu kufanya ukatili wa kingono kwa wanafunzi wa kike. Kwa kipindi cha mwaka 2019 hadi 2021, LHRC ilikusanya jumla ya matukio kama hayo 39. Ukiacha walimu kufanya vitendo vya ukatili wa kingono, matukio ya mimba na ndoa za utotoni pia yamekuwa yakiongezeka katika kipindi cha janga la Uviko19 (2020 na 2021).

> Zaidi ya wasichana 120,000 huacha shule kila mwaka nchini Tanzania, huku 6,500 kati yao wakiacha shule sababu ya mimba au kuwa na watoto.
> - Benki ya Dunia, 2021

Mojawapo ya mambo chanya katika sekta ya elimu kwa mwaka 2021 ilikuwa ni maamuzi ya Serikali kuruhusu wasichana wanaopata ujauzito kuendelea na masomo. Pia, kuna matumaini ya Serikali kutekeleza hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Rufani ya Tanzania katika Kesi ya Rebecca Gyumi na kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kuondoa ndoa za utotoni kwa kuweka umri wa chini wa kuoa na kuolewa kuwa miaka 18.

## 3.2. Haki ya Afya

Kwa mwaka 2021, Serikali ilichukua hatua mbalimbali kuhakikisha utekelezaji wa haki ya afya kulingana na rasilimali zilizopo, na kutatua baadhi ya changamoto katika sekta ya afya, ikiwemo utoaji na usambazaji wa vidonge, madawa, na vifaa tiba, pamoja na ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya na hospitali. Hata hivyo, kulikuwa na changamoto mbalimbali ambazo ziliathiri utekelezaji madhubuti wa haki ya afya, ikiwemo ufinyu wa bajeti; upungufu wa wafanyakazi; afya ya akili na watu kujiua; ukatili dhidi ya wanawake na wasichana; upungufu wa mashine, madawa, na vitaa tiba; na changamotzo zinazohusiana na afya ya uzazi.

### *Upungufu wa wafanyakazi, vituo vya afya/ hospitali*

- Mwaka 2021 iliripotiwa kwamba sekta ya afya ilikuwa inakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi kwa asilimia 52, kwa kuwa wafanyakazi waliopo walikuwa

ni asilimia 48 pekee. Katika Mkoa wa Dodoma, iliripotiwa kwamba kulikuwa na upungufu wa wafanyakazi kwa asilimia 67.


- Upungufu wa vituo vya afya ulitajwa pia kama changamoto kwa wanajamii, hasa katika maeneo ya vijijini, ambapo walikuwa wanalazimika kusafiri kwa umbali mrefu kufikia huduma za afya


### *Afya ya mama na mtoto*

- Upungufu wa wafanyakazi, upungufu wa sehemu kwa ajili ya wanawake wajawazito, upungufu wa vituo vya afya/hospitali, na ukatili dhidi ya wanawake na watoto vilitajwa kama baadhi ya vikwazo vya upatikanaji wa huduma za afya ya mama mwaka 2021. Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya matukio mawili ya ukatili majumbani ambao ulifanywa dhidi ya wanawake wajawazito. Iliripotiwa kwamba wanawake hao walifanyiwa ukatili wa kimwili na wenza wao, hususan kupigwa. Hali hii siyo nzuri, kwani ukatili kama huu hupelekea pia mimba kuharibika au kutoka.
- Kutokana na kutopatikana kwa huduma nzuri za afya katika baadhi ya maeneo, vifo vya mama na mtoto pia vimekuwa changamoto, hasa katika vituo vya afya maeneo ya vijijini, ambapo vifo vingi hutokea. Ndoa na mimba za utotoni, ambazo zimeendelea kushamiri katika baadhi ya mikoa nchini Tanzania, zinawaweka wasichana na vijana wa kike katika hatari ya kufariki wakati wa kujifungua.

### *Afya akili na watu kujiua*

- Kuongezeka kwa matukio ya watu kujiua mwaka 2021 kunaashiria uwepo wa changamoto ya afya ya akili. Katika mwaka huo, LHRC ilikusanya matukio 45 ya watu kujiua, yakiongezeka kutoka 22 mwaka 2020. Sababu za watu kujiua zilizotajwa katika matukio hayo ni pamoja na: mume kuachiwa baada ya kukamatwa na polisi na kuwekwa rumande; kukataliwa uhusiano wa kimapenzi; kuripotiwa na mke kituo cha polisi; kutuhumiwa kuiba; madeni; kutotambuliwa na mchungaji kanisani; mke kutishia kumuacha mume; wivu wa kimapenzi; kugundua mwenza na VVU; kukutwa na VVU; kutolipwa malimbikizo ya mshahara; na ugumu wa maisha.






- Asilimia kubwa ya watu waliojua katika matukio yaliyokusanywa na LHRC mwaka 2021, zaidi ya theluthi mbili (asilimia 76), ni wa kiume. Kwa upande wa umri, tathmini iliyofanywa na LHRC inaonyesha kwamba asilimia kubwa ya watu waliojiua mwaka 2021 (asilimia 42) walikuwa wana umri kati ya miaka 15 hadi 35 (vijana).

### *Bima ya afya*

- Kwa mwaka 2021, kukosekana kwa bima ya afya kwa baadhi ya Watanzania kuliendelea kuleta changamoto katika utekelezaji madhubuti wa haki ya afya. Zaidi ya nusu ya Watanzania hawana bima ya afya.

### *Afya ya uzazi na haki za afya ya uzazi*

- Utekelezaji wa haki za afya uzazi, hasa kwa upande wa vijana, uliendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo ukatili dhidi ya watoto na vijana; mtazamo hasi kuhusu baadhi ya vipengele vya afya ya uzazi; na kutopatikana kirahisi kwa taarifa sahihi kuhusu afya ya uzazi kulingana na umri wa watoto na vijana.
- Vikwazo vingine katika utoaji wa huduma za afya ya uzazi nchini Tanzania ni pamoja na upungufu wa wafanyakazi katika sekta ya afya, suala ambalo ni changamoto kubwa; foleni ndefu hospitalini na katika vituo vya afya; baadhi ya wafanyakazi kuwa na mtazamo hasi wakati wa utoaji wa huduma, ikiwemo kuwahukumu na kuwasema wateja; unyanyapaa na ubaguzi; mitazamo ya kidini; na dhana potofu kuhusu afya ya uzazi na huduma za uzuiaji wa VVU.
- Zaidi ya asilimia 90 ya walimu katika shule za msingi na sekondari nchini Tanzania wanadhani hawafundishi vya kutosha na kwa kina kuhusu afya ya uzazi na haki za afya ya uzazi.

## 3.3. Haki ya Maji

Pamoja na juhudi mbalimbali za kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa haki ya maji, bado kuna changamoto kubwa za upatikanaji wa maji safi na salama katika baadhi ya maeneo

nchini, ikiwemo katika Mikoa ya Mwanza, Kigoma, Kilimanjaro, Kagera, Shinyanga, na Mara. Changamoto nyingine zinazochangia pia kutopatikana kwa maji safi na salama ni pamoja na fedha za bajeti kutopatikana kwa wakati (ucheleweshaji); watu kuunga au kuungiwa maji kinyume na sheria; na uvujaji na upotevu wa maji.

## 3.4. Haki ya kufanya Kazi

Kwa mwaka 2021, masuala makubwa yaliyoathiri haki ya Watanzania kufanya kazi ni pamoja na: mzigo wa makato ya kodi ya wafanyakazi na makato ya mikopo ya elimu ya juu; upungufu wa wafanyakazi katika sekta za afya na elimu; mazingira yasiyoridhisha ya kufanyia kazi; wafanyakazi kutopata muda wa kutosha wa kumpumzika; na ukiukwaji wa haki za wafanyakazi, ambao uliongezeka kwa sababu ya janga la Uviko19.

### *Mzigo wa makato ya kila mwezi*

- Mzigo wa makato mbalimbali ya mwisho wa mwezi, ikiwemo makato ya kodi ya mfanyakazi na mikopo ya elimu ya juu, iliendelea kuwa changamaoto kwa wafanyakazi kati sekta za umma na binafsi, huku wengine wakikatwa kiwango kinachozidi theluthi mbili ya mshahara, kinyume na sheria. Changamoto hii ilionekana zaidi kwa wafanyakazi wa halmashauri mbalimbali zilizopo Tanzania Bara.

### *Mazingira ya kazi*

- Wafanyakazi katika sekta zinazotoa huduma, kama vile walimu na wafanyakazi katika sekta ya afya, waliathiriwa zaidi na mazingira yasiyoridhisha ya kazi. Kwa mfano, kwa upande wa walimu changamoto zilizoathiri mazingira yao ya kazi ni pamoja na upungufu wa madarasa, walimu, na nyumba za walimu, ambazo ziliathiri pia ubora wa elimu.

### *Kufanya kazi muda wa ziada*

- Kwa mwaka 2021, LHRC ilipokea taarifa mbalimbali za wafanyakazi kufanyishwa kazi muda wa ziada, kiasi cha kushindwa kupata muda wa kutosha wa kupumzika. Haya yalibainishwa katika utafiti kuhusu haki za binadamu na biashara uliofanyika katika mikoa 15 ya Tanzania Bara. Wafanyakazi ambao walionekana kuwa wahanga wakuu wa suala hili ni wale wa kwenye sekta za usafirishaji, ulinzi, na ukarimu (huduma za hoteli), kama vile madereva wa mabasi na malori, wafanyakazi wa hoteli, na walinzi.

***Ukiukwaji wa haki za wafanyakazi na migogoro ya kazi***

- Ukiukwaji wa haki za wafanyakazi na migogoro baina ya waajiri na wafanyakazi viliongezeka mwaka 2021, huku janga la Uviko19 likichangia katika hilo.
- Pia, utafiti wa haki za binadamu uliofanyika katika mikoa 20 ya Tanzania Bara ulibaini ukiukwaji wa haki za wafanyakazi katika sekta ya habari (wanahabari). Asilimia kubwa ya wanahabari walioshiriki katika utafiti huo (asilimia 73) walitaja kutopewa mkataba kama changamoto kubwa. Changamoto nyingine zilizotajwa ni pamoja na ujira mdogo/usio stahiki (asilimia 68), vitisho (asilimia 56), kufukuzwa kazi kinyume na sheria (asilimia 55), na ukiukwaji wa mkataba wa ajira unaofanywa na mwajiri (asilimia 54). Pia, unyanyasaji wa kingono na rushwa ya ngono kwa waandishi wa habari wanawake pia vilionekana kuwa changamoto kubwa (asilimia 42) na tatizo kiasi (40).

## 3.5. Haki ya Kumiliki Mali

Kwa mwaka 2021, masuala makuu yaliyoathiri utekelezai wa haki ya kumiliki mali ni pamoja na: migogoro ya ardhi; ukiukwaji wa haki za wanawake kutumia na kumiliki mali; unyang'anyi wa mali kutoka kwa wajane na wazee; na uandishi wa wosia kulinda haki za kumiliki mali na urithi.

***Haki za wazee na wanawake za kumiliki mali na urithi***


- Matukio ya ukiukwaji wa haki ya kumiliki mali na urithi yaliyoripotiwa ni pamoja na: kuwanyan'ganya mali wazee; watoto kulazimisha wazazi wao wazee kuwapatia mali au urithi, hadi kufikia kuwaua wazazi kufanikisha jambo hilo; na kuwanyan'ganya wajane mali walizochuma na waume zao.
- Kwa mwaka 2021, matumizi na umiliki wa ardhi viliendelea kuwa changamoto kwa upande wa wanawake, hasa katika maeneo ya vijijini ambapo sheria za kimila zinatumika.

***Migogoro ya ardhi***

- Mwaka 2021 migogoro ya ardhi, ikiwemo kati ya wakulima na wafugaji, ilindelea kuhatarisha utekelezaji wa haki ya kumiliki mali.
- Zaidi ya theluthi moja ya migogoro ya ardhi (39%) inahusiana na kutolipwa fidia, hasa kwa upande wa taasisi za umma.

***Uandikaji wa wosia kulinda haki zinazohusiana na mali***

- Japokuwa washiriki wengi wa utafiti (Watanzania wengi) wadhani kuandika wosia ni muhimu (asilimia 91), ili kulinda haki ya kumiliki mali, ni asilimia 11 pekee walisema wameandika wosia. Sababu za kutoandika wosia ni pamoja na kutokuwa na uelewa/uelewa mdogo (asilimia 66), dhana kwamba kuandika wosia ni kukikaribisha au kujichulia kifo (asilimia 37), na mtazamo kwamba umri wa kuandika wosia bado (asilimia 28).





*Sababu za watu kutoandika wosia*

*"Watu wanahisi ni uchuro watu hawana mwamko wa kuandika wosia. Hakuna watu wana tabia ya kuandika wosia, wanaogopa hawaelewi, wanaona ni uchoro .Tunaamini anayetakiwa kuaandika ni mtu mwenye mali mengi ila watu wengi hawaachi wosia...."*
**Mwanajamii, Geita**

## 3.6. Athari ya Uviko19 kwenye Haki za Kiuchumi na Kijamii

- Kama ilivyokuwa kwenye maeneo mengine ya haki za binadamu, Uviko19 pia uliathiri haki za kiuchumi na kijamii. Wanajamii walioshiriki katika utafiti wa haki za binadamu mwaka 2021 waliulizwa kuhusu namna ambavyo janga la Uviko19 liliathiri haki zao za kiuchumi na kijamii. Upotevu au upunguaji wa kipato ulitajwa kama changamoto kubwa zaidi (asilimia 93), ukifuatiwa na kulazimika kubadilisha chanzo cha kipato (asilimia 86), kukatisha masomo (asilimia 82), na kutopata huduma za kiafya kirahisi (asilimia 81). Athari nyingine zilizosababishwa na janga hilo ni pamoja na kuathirika kwa afya ya akili (asilimia 76), upungufu wa chakula (asilimia 72), na kupoteza ajira/kazi (asilimia 71).




*Athari za Uviko19 kwenye haki za kiuchumi na kijamii*



# 04

## SURA YA NNE:
## **HAKI ZA KIUJUMLA**

## SURA YA NNE:
# HAKI ZA KIUJUMLA

## Utangulizi

Kwa mwaka 2021, hatua iliyokuwa imepigwa katika utekelezaji wa haki za kiujumla kabla ya kuibuka kwa janga la Uviko19 zilirudishwa nyuma zaidi na athari ya janga hilo.

## 4.1. Haki ya Maendeleo

Utekekelezaji wa haki hii uliathiriwa na Uviko19. Pia, haki hii inategemea utekelezaji wa haki za kiraia, kisiasa, kijamii, kiuchumi, na kijamii, ambazo utekelezaji wake ulidodora mwaka 2021 kama ilivyokuwa mwaka 2020.

- Kama ilivyoelezewa katika Sura ya Pili hapo juu, haki za msingi za binadamu kama vile uhuru wa kujieleza, uhuru wa kukusanyika, na uhuru wa kujumuika, ziliendelea kuathiriwa na sheria zenye vifungu vinavyominya haki hizo kinyume na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, hasa kufuatia marekebisho mbalimbali ya kisheria yaliyofanyika mwaka 2019 na 2020. Changamoto hizi za kisheria pamoja na vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu vilivyofanywa na baadhi ya maafisa na viongozi wa Serikali, zimesababisha tushindwe kupiga hatua katika eneo la maendeleo ya kisiasa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.
- Janga la Uviko19 pia liliathiri maendeleo ya kijamii, ikiwemo kwa kuathiri utoaji madhubuti wa huduma za elimu na afya, pamoja na upotevu wa kipato na ajira.

- Kwa kusababisha upotevu wa kipato na ajira, Uvikio19 pia iliathiri maendeleo ya kibinadamu.

.

## 4.2. Haki ya Kufurahia na Kufaidika na Rasilimali asilia/ Maliasili

Kwa mwaka 2021, Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha utekelezaji wa haki ya kufurahia na kunufaika na rasilimali asilia/maliasili, ikiwemo kupitia ukusanyaji wa mapato katika sekta muhimu kama vile ya madini ili kuchangia katika maendeleo ya taifa. Hata hivo, janga la Uviko19 lilihakikisha haki hii haitekelezwi vizuri, ikiwemo katika sekta kama za utalii na viwanda. Changamoto nyingine zilizoathiri ufurahiaji na utekelezaji wa haki hii mwaka 2021 ni pamoja na rushwa na ukwepaji kodi, hasa katika sekta ya uchimbaji.

## 4.3. Haki ya Mazingira Safi na Salama

Haki ya mazingira safi na salama inahitaji uwepo wa mazingira salama, ikiwemo maji, hewa, na udongo safi, ambavyo havina sumu au madhara yoyote kwa binadamu. Mwaka 2021 ulikuwa ni mwaka wa kihistoria kwa upande wa haki ya mazingira safi na salama baada ya Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu kutangaza rasmi kwamba haki ya mazingira safi na salama ni haki ya binadamu.

> *Haki za binadamu na mazingira zinategemeana; haki za binadamu haziwezi kufurahiwa bila mazingira safi na salama; na pia utunzaji mzuri wa mazingira hauwezi kuwepo bila ya haki za binadamu kuheshimiwa. Uhusiano huu kati ya haki za binadamu na mazingira umeendelea kutambuliwa katika nchi mbalimbali kwa kuwa haki ya mazingira salama kwa sasa imejumuishwa katika katiba za nchi zaidi ya 100 duniani.*
>
> ***- Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP)***

Nchini Tanzania, Serikali imechukua hatua mbalimbali kusimamia, kutunza, na kulinda mazingira. Hata hivyo, changamoto mbalimbali zimekuwa zikipelekea haki ya mazingira safi na salama kukiukwa, hasa

changamoto ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira unaofanywa na biashara (hasa makampuni na viwanda) na watu binafsi. Katika kipindi cha mwaka 2020/21 LHRC ilikusanya takribani matukio 15 ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira, ikiwemo uchafuzi wa vyanzo vya maji, uchafuzi wa hewa, kelele, na uharibifu wa ardhi, ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Shinyanga, Dodoma, Mara, Tanga, Geita, Mtwara, Mbeya, na Pwani.

## 4.4. Athari ya Uviko19 kwenye Haki za Kiujumla

Kama ilivyoelezewa hapo juu, ufurahiaji wa haki za kiujumla unategemea ufurahiaji wa haki za msingi zilizojadiliwa katika sura za pili, tatu, na tano za ripoti hii. Hivyo basi, athari ya Uviko19 kwenye haki hizo, kama ilivyoelezewa katika sura hizo, ilisababisha pia athari kwenye haki za kiujumla. Sekta kama vile za utalii na ukarimu ziliathiriwa zaidi na janga la Uviko19, ikiwemo kupitia upotevu wa ajira, kupungua kwa kipato, na upotevu au upunguaji wa mapato kwa upande wa Serikali. Pia, utoaji wa huduma za msingi za kijamii, hasa huduma za afya,uliathiriwa sana na Uviko19, hivo pia kuathiri maendeleo ya kijamii.



05

SURA YA TANO:

# HAKI ZA MAKUNDI MAALUM


## SURA YA TANO:
# HAKI ZA MAKUNDI MAALUM

### Utangulizi

Baadhi ya makundi katika jamii yapo katika hatari zaidi ya kufanyiwa vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu kuliko mengine. Kwa kulitambua hili, makundi haya yamepatiwa ulinzi maalum, ambapo kuna mikataba na sheria mbalimbali ambazo zinalinda haki za makundi hayo. Kwa upande wa Tanzania, makunid haya maalum ni pamoja na wanawake, watoto, watu wenye ulemavu, wazee, watu wanaoishi na VVU/UKIMWI, na wakimbizi.

### 5.1. Haki za Wanawake

Ukiacha mikataba mbalimbali ya haki za binadamu inayotoa ulinzi wa haki za binadamu kwa watu wote, kuna mikataba kadhaa ambayo ni ya haki za wanawake pekee. Mikataba hii ni pamoja na Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa mwaka 1979 na Mkataba wa Afrika wa Haki za Wanawake (Maputo Protocol) wa mwaka 2003. Jambo kubwa linalokatazwa katika mikataba hii ni ubaguzi dhidi ya wanawake unaopelekea kushindwa kufurahia haki zao muhimu kama binadamu. Pia, mikataba hii inakataza ain azote za ukatili wa kijinsia.





*Asilimia ya wahanga wa ukatili wa kijinsia nchini Tanzania – Jan. hadi Dis. 2021*

### Mienendo ya Ukatili wa Kijinsia na Ukatili dhidi ya Wanawake

Kwa mwaka 2021, masuala muhimu yaliyoathiri haki za wanawake ni pamoja na:

ukatili wa kimwiil; ukatili wa kingono, hasa ubakaji na ulawiti; ukatili wa kisaikolojia; na rushwa ya ngono.

- Kwa mwaka 2021, takwimu za jeshi la polisi zilionyesha kwamba jumla ya matukio 11,138 ya ukatili wa kijinsia yaliripotiwa, sawa na punguzo la matukio 8,670. Pamoja na kupungua kwa matukio hayo, bado tatizo la ukatili dhidi ya wanawake ni kubwa, kwani ni sawa na wastani wa matukio 928 kila mwezi. Hii ni sawa na wanawake 30 kufanyiwa aina tofauti ya vitendo vya ukatili kila siku. Ikumbukwe pia kwamba kuna matukio mengi ya ukatili huwa hayaripotiwi.
- Kwa upande mwingine, takwimu zilizotolewa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum zinaonyesha kwamba idadi ya wanawake ambao walikuwa wahanga wa ukatili wa kijinsia kwa mwaka 2021 ilikuwa ni 20,897, kama inavyoonyeshwa katika chati hapo chini.




*Wahanga wa ukatili wa kijinsia nchini Tanzania kwa jinsi - 2017 hadi 2021*

Kati ya matukio 29,373 ya ukatili wa kijinsia yaliyoripotiwa mwaka 2021, matukio 12,817 (44%) yaliripotiwa katika Mikoa ya Kipolisi ya Arusha, Ilala, Tanga, Kinondoni, na Rukwa pekee (ama Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Tanga, na Rukwa).

### *Mitazamo ya wanajamii kuhusu ukatili wa kijinsia/ukatili dhidi ya wanawake*

- Nusu ya washiriki wa utafiti wa haki za binadamu (52%) walidai kwamba ukatili dhidi ya wanawake ni tatizo kubwa katika jamii yao, wakifuatiwa kwa karibu na wale waliodai kwamba ni tatizo kiasi (41%).

### *Aina na vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake vinavyoripotiwa zaidi*


- Aina na vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake vilivyoripotiwa zaidi mwaka 2021 ni ubakaji, ulawiti, ukatili dhidi ya mwenza/ukatili wa majumbani (hasa vipigo), matusi/udhalilishaji, kuumizwa vibaya au kuuwawa na mwenza sababu ya wivu wa kimapenzi, kuuwawa sababu ya imani za kishirikina, kunyimwa urithi au kumiliki mali, kushikwa sehemu mbalimbali za mwili bila ridhaa au unyanyasaji wa kingono, na rushwa ya ngono.
- Vitendo hivi vya ukatili dhidi ya

wanawake vinafanywa zaidi na wenza wao, ama mume au mpenzi. Watu wengine wanaodaiwa kufanya vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake ni pamoja na wanafamilia, hasa ndugu wa mume, ambao wanadaiwa pia kuwanyanyasa na kuwafanyia vitendo vya ukatili wajane.

### *Vyanzo/visababishi vya ukatili dhidi ya wanawake*

- Umaskini au ukosefu wa kipato kwa wanawake uliendelea kutajwa kama mojawapo ya vyanzo au visababishi vikuu vya ukatili dhidi ya wanawake. Hii ni kwa sababu baadhi ya wanawake wanahisi kwamba hawana jinsi zaidi ya kuendelea kukaa na wenza wao wanaowafanyia vitendo vya ukatili kwa sababu ya kutokuwa na kazi au shughuli ya kiuchumi ya kuwaingizia kipato. Vyanzo au visababishi vingine vya ukatili dhidi ya wanawake ni pamoja na mfumo dume katika jamii; ulevi, hasa kwa upande wa wenza wao; tabia au utamaduni wa kusuluhisha migogoro katika ngazi ya familia; imani za kishirikina; uelewa mdogo kuhusu haki za binadamu na ukatili wa kijinsia; mila na tamaduni baguzi, ikiwemo zinazowanyima wanawake haki ya kurithi na kumiliki ardhi; mahusiano nje ya ndoa; na ukatili kuvumiliwa na kuonekana ni jambo la kawaida.

Mikoa 5 (ya kipolisi) iliyoongoza kwa Ukatili wa Kijinsia Tanzania mwaka 2021




*Chanzo*: Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, 2022

*"Kuna mwanaume mmoja katika Kata ya Lukobe ambaye humpiga mkewe na mwanae wa kiume mara kwa mara. Lakini kila mara anapokamatwa na polisi mke wake huomba sana aachiwe kwa sababu ndiye mleta mkate pekee au mwenye kipato katika familia."*
**- Afisa Ustawi wa Jamii, Manispaa ya Morogoro**

### *Ukatili dhidi ya mwenza na mauaji ya mweza*

- Ukatili dhidi ya mwenza, ambao wakati mwingine hupelekea kifo cha mwenza, umekuwa tishio kwa haki za


wanawake nchini Tanzania katika miaka ya hivi karibuni na matukio ya aina hii yaliendelea kuripotiwa mwaka 2021. Katika mwaka huu, LHRC ilikusanya jumla ya matukio 35 ya mauaji yaliyosababishwa na ukatili dhidi ya mwenza, wahanga wengi (89%) wakiwa ni wanawake. Jumla ya wanawake 31 waliouwawa na wenza wao, sawa na punguzo la tukio 1 ukilinganisha na mwaka 2020. Kati ya watu 35 waliouwawa na wenza wao, asilimia 72 waliuwawa kwa sababu ya wivu wa kimapenzi.




*Mwanamke mmoja mkoani Rukwa ambaye mpenzi wake alimkata masikio sababu ya wivu wa kimapenzi*

### Ukatili wa kimwili dhidi ya wanawake

- Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya takribani matukio 70 ya ukatili wa kimwili dhidi ya wanawake, ambayo ni sawa na ongezeko la matukio mara tatu ukilinganisha na matukio yaliyokusanywa mwaka 2020. Matukio haya yaliripotiwa katika mikoa mbalimbali, ikiwemo Katavi, Kilimanjaro, Geita, Tabora, Shinyanga, Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Pwani, na Mara. Wahanga walifanyiwa aina hii ya ukatili kwa sababu mbalimbali, ikiwemo imani za kishirikina, tendo la ndoa, wivu wa kimapenzi, kugombania mtoto, ugonjwa wa muda mrefu, na ulevi.
- Zaidi ya nusu ya wanajamii walioshiriki kaitka Utafiti wa Haki za Binadamu wa mwaka 2021 (54%) walisema kwamba ukatili wa majumbani ni tatizo kubwa katika jamii yao.




*Mitazamo ya washiriki wa utafiti (wanajamii) kuhusu tatizo la ukatili wa majumbani*

### *Ukatili wa kingono dhidi ya wanawake*

- Ukatili wa kingono ulendelea kuwa tatizo kubwa kwa wanawake katika maeneo mbalimbali ya Tanzania mwaka 2021. LHRC ilikusanya takribani matukio 51 ya ukatili wa kingono dhidi ya wanawake kwa upande wa Tanzania Bara, sawa na matukio 19 pungufu ya yale yaliyokusanywa mwaka 2020. Matukio mengi yalikuwa ni ya ubakaji, ambayo yaliripotiwa katika mikoa tofauti, ikiwemo, Mwanza, Dar es Salaam, Morogoro, Lindi, Mara, Tabora, Dodoma, Pwani, Mbeya, Katavi, Manyara, na Tanga.
- Mwaka 2019, idadi ya matukio ya ubakaji yaliyoripotiwa polisi yalikuwa 7,837, ambayo yalipungua hadi matukio 7,263 mwaka 2020. Kwa mwaka 2021, idadi ya matukio ya ubakaji yaliyoripotiwa polisi yalipungua zaidi hadi kufikia matukio 6,305, sawa na punguzo la matukio 958 au asilimia 13.2.
- Unyanyasaji wa kingono pia ulitajwa kama mojawapo ya aina za ukatili dhidi ya wanawake inayotokea zaidi katika jamii, ikiwemo kwa wanahabari wanawake. Zaidi ya theluthi moja ya wanajamii walioshiriki katika utafiti wa haki za binadamu uliofanywa na LHRC (asilimia 35) walisema kwamba unyanyasaji wa kingono ni tatizo kubwa katika jamii, huku karibia nusu ya washiriki (asilimia 43) wakisema ni tatizo kiasi.
- Mwaka 2021 rushwa ya ngono haikuwa mwiba tu kwa wanawake walio katika sekta ya habari, bali pia katika maeneo mengine kama vile soko la ajira, katika taasisi za elimu ya juu, na katika utoaji wa huduma mbalimbali. LHRC ilikusanya matukio manne ya rushwa ya ngono, ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Kagera, Dodoma, na Morogoro. Hata hivyo, bado kuna matukio mengi ambayo huwa hayaripotiwi, hasa pale ambao rushwa ya ngono haijatolewa. Karibia nusu ya wanajamii walioshiriki katika utafiti wa haki za binadamu (asilimia 42) walisema kwamba rushwa ya ngono ni tatizo kubwa katika jamii zao.

### *Ukatili dhidi ya wanawake katika sekta ya habari*

- Kuhusu ukatili dhidi ya wanawake katika sekta ya habari, karibia nusu ya wanahabari walioshiriki katika utafiti (asilimia 42) walisema ukatili dhidi ya wanawake katika sekta hiyo ni tatizo kubwa, wakifuatiwa na asilimia 40 waliosema kwamba ni tatizo kiasi. Aina za vitendo vya ukatili dhidi ya wanahabari wanawake ambavyo

hutokea zaidi ni pamoja na kuombwa rushwa ya ngono; kushikwa sehemu za mwili bila ridhaa, hasa matiti na matako; kuonyeshewa ishara za kingono au kuambiwa maneno ya kingono; kushikwashikwa mikono bila ridhaa au kujigusisha kwenye mwili wa mwanamke au kuzuia asipite; kumtongoza au kumtaka kilazima mwanamke; na mwanaume kutaka mwanamke kutoka nae mara kwa mara.

- Wahariri na maafisa rasilimali watu walitajwa zaidi kama wafanyaji wa vitendo vya ukatili wa kingono dhidi ya wanahabari wanawake. Wengine waliotajwa na washiriki wa utafiti ni pamoja na wakurugenzi/mameneja, wamiliki wa vyombo vya habari, na vyanzo vya habari. Adhabu ya kukataa maombi ya rushwa ya ngono ni pamoja na kukosa ajira, kuwekewa mazingira magumu ya kufanya kazi, kutochapisha habari ya mhanga, na kufukuzwa kazi kinyume na sheria.

### *Ukatili wa kiuchumi dhidi ya wanawake*

- Aina mbalimbali za ukatili wa kiuchumi dhidi ya wanawake ziliripotiwa katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara mwaka 2021. LHRC ilikusanya takribani matukio 77 ya ukatili wa kiuchumi dhidi ya wanawake, ambayo ni pamoja na ya kuingilia haki ya wanawake ya kupata na kumiliki mali, kuhakikisha mwanamke hashiki au hapati fedha, na kunyimwa urithi. Kwa mwaka 2020, LHRC ilikusanya matukio 27 ya ukatili wa kiuchumi dhidi ya wanawake.

*"…wanawake wa Mkoa wa Mara hawathaminiki kabisa, hawana haki ya kumiliki ardhi hasa pale wazazi au wenza wao wakifariki hawarithi mali…mimi nina jirani yangu mjane, baada ya mume wake kufariki ndugu wa mwanaume wamemfukuza kwenye nyumba ambayo alijenga yeye na mume wake wakimwambia hana haki tena ya kukaa kwenye hiyo nyumba…kesi sasa iko Mahakamani…"*
**Mwanajamii, Mara**

- Kwa mwaka 2021, matukio kadhaa ya wanawake kufukuzwa nyumbani yaliripotiwa kama mojawapo ya aina za ukatili wa kiuchumi dhidi ya wanawake zinazotokea zaidi katika jamii. Kupitia programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu na utafiti wa matukio ya haki za binadamu yanayoripotiwa na vyombo vya habari, LHRC ilikusanya matukio 23 ya wanawake kufukuzwa nyumbani wanapoishi na waume zao. Matukio hayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Mwanza, Manyara, Songwe, Mara, Morogoro, Mbeya na Rukwa.

### *Ukiukwaji wa haki za wajane za kumiliki mali na urithi*

- Matukio ya wajane kunyang'anywa mali mara baada ya waume zao kufariki yamekuwa yakitoea sana nchini Tanzania, hasa maeneo ya vijijini ambapo sheria za kimila hutumika zaidi. Kwa kipindi cha miaka ya 2020 na 2021, LHRC ilikusanya jumla ya matukio 42 ya ukiukwaji wa haki za wajane za kumiliki na kurithi mali kwa kufukuzwa katika nyumba walizokuwa wanaishi na waume zao na kunyimwa urithi. Matukio 16 kati ya haya yaliripotiwa mwaka 2020, huku 26 yaliyobakia yakiripotiwa mwaka 2021.

### *Ushiriki wa wanawake katika siasa*

- Tanzania ni mojawapo ya nchi nyingi duniani ambazo zimepiga hatua katika kukuza ushiriki wa wanawake katika siasa na kulinda haki zao za kisiasa miaka 26 tangu Azimio la Beijing la mwaka 1995. Kwa sasa Tanzania ina Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye aliweka historia mwaka 2021 kwa kuwa Rais mwanamke wa kwanza nchini Tanzania. Hata hivyo, kasi ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika siasa na uongozi katika nchi mbalimbali duniani, ikiwemo Tanzania, imekuwa ndogo. Hali hii imesababisha kushindwa kufikia malengo mbalimbali ya usawa wa kijinsia katika siasa na nafasi za uongozi.

**Asilimia ya wanawake wanaoshika nafasi mbalimbali za uongozi katika ofisi za umma (kufikia mwezi Machi 2022)**

| Nafsi | Idadi ya Wanawake | Asilimia ya Wanawake |
|---|---|---|
| Mawaziri | 8 kati ya 22 | 36 |
| Manaibu Waziri | 5 kati ya 23 | 22 |
| Makatibu Wakuu | 3 kati ya 21 | 14 |
| Wakuu wa Mikoa | 6 kati ya 26 | 23 |
| Makatibu Tawala Mkoa | 22 kati ya 26 | 46 |

- Vikwazo vikuu kwa ushiriki wa wanawake katika siasa na uwakilishi katika nafasi za uongozi ni pamoja na: mianya ya kijinsia katika sheria za uchaguzi, ikiwemo Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977; ukatili dhidi ya wanawake katika siasa/chaguzi; mila na tamaduni zinazobagua au kuwakandamiza wanawake; kukosa rasimali fedha; kutopata msaada wa kutosha kutoka kwa vyama vya siasa na kutoshirikishwa vya kutosha na kupata uwakilishi wa kutosha katika maamuzi yanayofanywa ndani ya chama; mianya ya kijinsia katika nyaraka za vyama

vya kisiasa kama vile katiba na ilani; na vyombo vya habari kutowapatia nafasi sawa na wagombea wa kiume, sambamba na kuwaonyesha au kuwaelezea katika mtazamo hasi.

***Uwezeshaji wanawake kiuchumi***

- Uwezeshaji wawanake kiuchumi ni silaha kubwa katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia. Nchini Tanzania uwezeshaji wanawake kiuchumi ni pamoja na utoaji wa mikopo isiyo na riba, kama asilimia 10 ya mapato ya halmashauri ambayo hutolewa kama mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu. Baadhi ya changamoto ambazo zimebainishwa katika utoaji wa mikopo hiyo ni pamoja na kutorejesha mikopo kwa wakati, kutokuwa na stadi/mbinu za ujasiriamali, wanavikundi kutoaminiana na kugombana mara kwa mara, na wanasiasa kuingilia mchakato wa utoaji wa mikopo hiyo.

***Wanawake na haki jinai***

- Wanawake, wakiwemo wafungwa na mahabusu, wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika mfumo wa haki jinai, ikiwemo ufikiaji wa haki, hali isiyoridhisha ya magerezani, na magereza/mahabusu kutozingatia mahitaji ya kijinsia. Mathalani, hali ya kutokuwa na rasilimali na ukatili wa kiuchumi ambao wanawake hufanyiwa huwaweka katika hatari ya kuzama katika umaskini na hivyo kushindwa kumudu gharama katika haki jinai, ikiwemo gharama za dhamana na uwakilishi mahakamani (wakili).

## 5.2. Haki za Watoto


Haki za watoto zinalindwa katika mikataba mikubwa miwili ya haki za watoto, ambayo ni: Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto (CRC) wa mwaka 1989 na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) wa mwaka 1990, yote ikiwa imeridhiwa na Tanzania. Kwa hapa nchini Tanzania pia tuna Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ambayo inataja haki za msingi za mtoto kama zilivyoelezewa kwenye mikataba hiyo na kueleza wazi kwamba katika kufanya maamuzi yoyote kuhusu mtoto kanuni ya maslahi bora ya mtoto lazima izingatiwe. Mikataba hii na sheria ya mtoto inatoa wajibu kwa Serikali, wazazi, walezi na wanajamii kwa ujumla kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyote vya ukatili na ubaguzi.

Kwa mwaka 2021, masuala makuu yaliyoathiri haki za watoto ni pamoja na: ukatili wa kingono; ukatili wa kimwili na kisakolojia; ajira kwa watoto na

utumikishwaji wa watoto; usafirishaji haramu wa watoto; ndoa za ututoni; na mimba za utotoni.


### *Mienendo ya ukatili dhidi ya watoto*

- Takwimu za polisi za mwaka 2021 zinaonyesha kwamba matukio ya ukatili dhidi ya watoto yalipungua kutoka 15,870 mwaka 2020 hadi 11,499 mwaka 2021, sawa na punguzo la asilimia 27.5. Asilimia 85 ya wahanga wa matukio hayo 11,499 walikuwa ni watoto wa kike, huku asilimia 15 iliyobaki wakiwa watoto wa kiume.
- Wasichana wameendeelea kuwa wahanga wakubwa wa ukatili dhidi ya watoto. Katika kipindi cha mwaka 2017 hadi 2021 kumekuwa na jumla ya wahanga wa kike 57,076 wa ukatili dhidi ya watoto, huku wahanga wa kiume wakiwa 13,921. Wahanga wa kike ni karibia mara nne ya wahanga wa kiume.




*Wahanga wa ukatili dhidi ya watoto kwa jinsi – 2017 to 2021*

Mikoa 5 Iliyoongoza kwa Matukio ya Ukatili dhidi ya Watoto mwaka 2021





*Chanzo*: Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, 2022

- Matukio 2,993 kati ya 11,499 yaliyoripotiwa polisi mwaka 2021, sawa na asilimia 26, yaliripotiwa katika Mikoa ya Arusha, Tanga, Shinyanga, Mwanza, na Mkoa wa Kipolisi wa Ilala (katika Mkoa wa Dar es Saaam).

### *Mitazamo ya wanajamii kuhusu ukatili dhidi ya watoto na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ambavyo hutokea zaidi*

- Zaidi ya nusu ya washiriki wa Utafiti wa Haki za Binadamu mwaka 2021 (asilimia 55) walisema ukatili dhidi ya watoto ni tatizo kubwa katika jamii zao. Utelekezaji wa watoto (asilimia 55) ulitajwa kama kitendo cha ukatili dhidi ya watoto kinachotokea zaidi, ukifuatiwa na vipigo/utesaji (asilimia


54), matusi/udhalilishaji (asilimia 50), na ubakaji (asilimia 48).




*Mtazamo wa wanajamii kuhusu vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ambavyo hutokea zaidi katika jamii zao*

### Matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyokusanya na LHRC

- Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya matukio mbalimbali ya ukatili dhidi ya watoto kupitia utafiti wa matukio yanayohusiana na haki za binadamu yaliyoripotiwa na vyombo vya habari. Asilimia 89 ya matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyoripotiwa yalikuwa ni ya ukatili wa kingono, huku asilimia 11 iliyobaki yakiwa ni ya ukatili wa kimwili na kisaikolojia. Matukio mengi yaliripotiwa katika Kanda ya Ziwa na Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, na Morogoro. Umri wa wahanga wa ukatili wa kingono dhidi ya watoto ulikuwa ni miaka 3 hadi 17..




*Matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyoripotiwa na vyombo vya habari*

### Wafanyaji wa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto

- Katika Utafiti wa Haki za Binadamu wa mwaka 2021 uliofanywa na LHRC, wanajamii walioshiriki katika utafiti huo waliwataja ndugu wa karibu/ wanafamilia kama wafanyaji wakuu wa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto (asilimia 66), wakifuatiwa na akinababa (asilimia 47), akinamama (asilimia 35), madereva bodaboda (asilimia 31), watu wasiojulikana (asilimia 30.3), na majirani (asilimia 27). Washiriki hao

pia walisema kwamba vitendo vya ukatili dhidi ya watoto hutokea zaidi nyumbani (asilimia 73), pakifuatiwa na mitaani (asilimia 70), na njiani kwenda shule (asilimia 38).

### *Sababu za kushamiri kwa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto*

- Kupitia tafiti mbalimbali zilizofanyika mwaka 2021, ikiwemo Utafiti wa Haki za Binadamu wa mwaka 2021, LHRC iligundua sababu mbalimbali za kushamiri kwa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Sababu hizo ni pamoja na familia za wahanga kutaka kuzizungumzia kesi za ukatili na 'kuzimaliza' katika ngazi ya familia, umbali mrefu kwenda shule, watoto kuachwa peke yao nyumbani kwa muda mrefu, malezi duni, ulevi, ugumu wa maisha, ndoa za utotoni, wazazi kutengana, na imani za kishirikina.

*"…unaweza kusikia mtu kabaka, ila ukifuatilia mbakaji kunakuwa na kumalizana na fidia, fidia inategemea na ukoo inaweza kwa ngombe, mbuzi au fedha kama laki 1 au laki 2. Kwa ng'ombe wanaweza kuwa 4 au 5 kutokana na msimamo wa familia na mila zao. Ukifuatilia polisi unakuta walalamikaji hawafiki"*

**VEO, Kilosa - Morogoro**

*"….watoto wa kike wanakatisha kwenye mapori kwenda shule ambazo zipo mbali na wanapokaa, hii ni hatari tunasikia wengine wanabakwaga kwenye misitu huko….."*

**Mfanyakazi shirika la kijamii, Kisarawe - Pwani**

### *Ukatili dhidi ya watoto mitandaoni*

- Mwaka 2021 ukatili dhidi ya watoto mitandaoni ulionekana kuwa changamoto kwa ulinzi wa haki za watoto, ikiwemo uhuru dhidi ya ukatili. Utafiti uliofanywa na mashirika ya kimataifa yanayojihusha na ulinzi wa haki za watoto ya ECPAT na UNICEF kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Polisi (INTERPOL) ulionyesha kwamba takribani watoto 200,000 walifanyiwa vitendo vya ukatili na utumikishwaji mitandaoni nchini Tanzania mwaka 2021. Mathalani, asilimia 3 ya watoto wanaotumia mtandao wa intaneti wenye umri wa miaka 12 hadi 17 walidai kuahidiwa fedha au zawadi kama watakutana wa watu wazima na kufanya nao vitendo vya kingono; asilimia 2 ya watoto walioshiriki katika utafiti huo walisema waliahidiwa kupewa fedha au zawadi kama wakituma picha zao za utupu; na asilimia 3 waliombwa kutuma picha na video zinazoonyesha utupu wao.

### *Ukatili wa kingono dhidi ya watoto*

- Kwa mwaka 2021 ukatili wa kingono dhidi ya watoto, hasa vitendo vya ubakaji na ulawiti, uliendelea kuwa tishio kubwa zaidi kwa haki za watoto. Wahanga wa aina hii ya ukatili dhidi ya watoto ni pamoja na watoto wenye miaka hadi 3.
- Tafiti zilizofanywa na LHRC mwaka 2021 zilionyesha kwamba watu walio karibu na watoto ndiyo wafanyaji wakuu wa vitendo vya ukatili wa kingono dhidi ya watoto. Watu hao ni pamoja na wanafamilia, wajomba, baba wa kambo, na akinababa. Madereva bodaboda na walimu wa kiume pia walitajwa kama mojawapo ya wafanyaji wa vitendo vya ukatili wa kingono dhidi ya watoto. Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya matukio 10 ya walimu wa kiume ambao walidaiwa kufanya ukatili wa kingono dhidi ya watoto/wanafunzi wa kike.
- Miongoni mwa matukio ya kusikitisha ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto yaliyoripotiwa mwaka 2021 ni pamoja na tukio moja la msichana mwenye miaka 14 ambaye alibakwa na kulawitiwa mande mkoani Katavi, na wasichana watatu wenye miaka 5, 14, na 6 ambao walibakwa na kisha kuuwawa katika Mikoa ya Manyara, Mara, na Mbeya.
- Watoto wa kiume pia walifanyiwa vitendo vya ukatili wa kingono, husasan ulawiti. Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya matukio 14 ya ulawiti wa watoto wa kiume, ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Tanga, Katavi, Mara, Manyara, Dodoma, Dar es Salaam, Morogoro na Njombe. Matukio manne kati ya haya yaliripotiwa katika Mkoa wa Katavi, ambapo katika mojawapo ya matukio hayo lilikuwepo tukio la mtoto wa miaka 13 kulawitiwa na kisha kuuwawa.
- Watoto waliripotiwa pia kufanyiana ukatili wa kingono mwaka 2021, ambapo matukio ya ukatili dhidi ya watoto unaofanywa na watoto yaliripotiwa katika mikoa kama vile Kagera, Dar es Salaam, Mbeya, na Lindi. LHRC ilikusanya jumla ya matukio 12.

### *Utumikishwaji wa watoto kingono*

- Matukio ya utumikishwaji wa watoto kingono pia yaliripotiwa kama mojawapo ya aina za ukatili ambazo watoto wa kike wanafanyiwa. Aina hii ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto iliripotiwa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Morogoro, ambapo baadhi ya wazazi na walezi walidaiwa kushiriki katika kuwatumikisha watoto kingono kwa ajili ya kujipatia fedha.


### *Ukatili wa kimwili na kisaikolojia dhidi ya watoto*

- Kwa mwaka 2021, ukatili wa kimwili uliripotiwa kama aina nyingine ya ukatili ambayo watoto hufanyiwa zaidi baada ya ukatili wa kingono. Matukio ya ukatili wa kimwili na kisaikolojia yaliripotiwa katika mikoa yote ambayo utafiti ulifanyika, ikiwemo Pwani, Morogoro, Kagera, Mara, na Geita.
- Kupitia utafiti wa matukio yanayoripotiwa na vyombo vya habari na programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu, LHRC ilikusanya takribani matukio 57 ya ukatili wa kimwili na kisaikolojia dhidi ya watoto. Matukio haya yaliripotiwa katika Mikoa ya Kagera, Rukwa, Mtwara, Ruvuma, Singida, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Geita, Shinyanga, Mbeya, na Arusha.
- Utafiti uliofanywa na LHRC mwaka 2021 ulionyesha kwamba wazazi wengi wanapenda kutoa adhabu ya kuchoma mikono pale ambapo watoto wao wamekosea. Mwaka 2021, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mh. Khamis Chilo, alisema katika mojawapo ya vikao Bungeni kwamba jumla ya watoto 130 (wa kiume 33, wa kike 97) walifanyiwa ukatili wa kimwili wa kuchomwa mikono katika kipindi cha mwezi Januari hadi Septemba 2021. Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Disemba 2021, LHRC ilikusanya takribani matukio 17 ya aina hii ya ukatili, ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Mara, Mtwara, Singida, Shinyanga, Katavi, na Dar es Salaam.
- Baadhi ya vitendo vya ukatili wa kimwili dhidi ya watoto vilivyoripotiwaa mwaka 2021 yalisababisha vifo. LHRC ilikusanya matukio sita ya ukatili wa kimwili dhidi ya watoto ambayo yalisabaisha vifo. Matukio haya yaliripotiwa katika Mikoa ya Katavi, Manyara,Tabora, Kigoma, Shinyanga, na Mara. Wahanga wengi walikuwa ni watoto wa kiume.
- Katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na matukio ya wazazi kuuwa watoto wao. Matukio haya yamekuwa yakiripotiwa katika maeneo mbalimbali duniani, ikiwemo Tanzania. Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya matukio mawili ya wazazi kuuwa watoto wao, ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Geita na Simiyu.

### *Ukatili wa kimwili na adhabu kali ya viboko*

- Kama ilivyo katika nchi nyingine nyingi barani Afrika, adhabu kali ya viboko imeendeela kuwa changamoto nchini Tanzania. Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya matukio saba ya adhabu kali za viboko kwa watoto mashuleni,

ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Mwanza, Morogoro, Dar es Salaam, Shinyanga, na Ruvuma. Adhabu hizo kali za viboko zilizababisha maumivu makali/madhara mwilini (5) na vifo (2). Kati ya wahanga saba wa adhabu kali ya viboko, wanne walikuwa wa kike na watatu wa kiume.




*Matukio ya adhabu kali ya viboko yaliyokusanywa na LHRC-2017 hadi 2021*

### *Ajira kwa watoto na utumikishwaji wa watoto*

- Washiriki wa utafiti wa haki za binadamu katika mikoa kama vile Dar es Salaam, Morogoro, na Kagera walisema kwamba ajira kwa watoto na utumikishwaji wa watoto ni tatizo katika jamii yao. Ufafiti kuhusu haki za binadamu na biashara, ambao nao ulifanywa na LHRC katika miezi ya Machi na Aprili mwaka 2021, ulionyesha kwamba ajira kwa watoto ni changamoto katika ulinzi wa haki za watoto, hasa katika Mikoa ya Manyara, Tabora, Singida, Mbeya, Geita, Shinyanga, na Dodoma.

*"..kuna malalamiko mengi yaliletwa na walimu juu ya wanafunzi kutofika shule kutokana na kupewa ajira ya kufukuza ndege kwenye mashamba ya mpunga. Wakulima wengi wa mpunga wanapenda kuwatumia watoto kwa sababu mpunga unaitaji kuinama katika kupanda kwake hivyo watu wazima wanashindwa na hawapandi vizuri ukilinganisha na watoto."*

**Afisa Mtendaji Kata – Wilaya ya Mbarali, Mbeya**



*Mtoto mwenye miaka 6 aliyekutwa anauza mbogamboga wakati wa masaa ya shule mkoani Ruvuma, Februari 2021*

- Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya matukio 48 ya ajira kwa watoto na utumikishwaji wa watoto ambayo yaliripotiwa katika karibia mikoa yote iliyopo Tanzania Bara, ikiwemo Morogoro, Iringa, Dodoma, Dar es Salaam, Geita, Mbeya, Tanga, na Songwe.

### *Ukatili dhidi ya watoto wanaofanya kazi za ndani*

- Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya matukio mawili ya ukatili dhidi ya watoto wanaofanya kazi za ndani, hasa wasichana, ambao walisafirishwa kiharamu kutoka Dodoma kwenda kufanya kazi jijni Dar es Salaam. Mkoani Morogoro, utafiti ulibaini kwamba wasichana wanaofanya kazi za ndani wanakumbana na changamoto mbalimbali, ikiwemo ukatili wa kiuchumi na ukatili wa kingono.

*"Wasaidizi wa kazi za ndani 'housegirls' wamekuwa na 'risk' nyingi kwani wanafanyiwa ukatili wa kutisha kama matusi, vijana wa mabosi wanawalazimisha kutembea nao, pia hata mume wa mama hapo nyumbani anaweza kumlazimisha kutembea nae pamoja na wageni mbalimbali wanaofika hapo nyumbani na hawana pa kusemea. Pia ni wachache sana wanaowalipa 'housegirls' kama makubaliano yalivyo, mara nyinyi mabosi wanawashawishi kuwawekea pesa zao kwa kuwaambia hawana matumizi nazo, sasa tatizo zikishakuwa nyingi wanatafuta sababu mfano anaweza kusema nakukata kiasi fulani cha pesa kwa sababu kuna kifaa ulivunja au kama kuna kutu fulani alimnunulia"*

**Msaidizi wa kisheria, Morogoro**

### *Utelekezaji watoto*

- Katika muktadha wa Tanzania, utelekezaji watoto ni aina ya ukatili dhidi ya mtoto, kwani husababisha mtoto asipate mahitaji muhimu kama vile chakula na mavazi, pia kulindwa dhidi ya ukatili. Kwa mwaka 2021, utelekezaji wa watoto uliendelea kuhatarisha ulinzi wa haki za watoto. Katika utafiti wa haki za binadamu uliofanywa na LHRC katika mikoa 20 ya Tanzania Bara mwaka 2021, utelekezaji wa watoto ulitajwa kama kitendo kikuu cha ukatili dhidi ya watoto (asilimia 60). Utelekezaji wa watoto pia ulitajwa kama changamoto kubwa wakati wa mahojiano na baaadhi ya washiriki wa utafiti.
- Mwaka 2021 LHRC ilikusanya matukio 24 ya utelekezaji wa watoto ambayo yaliripotiwa katika sehemu mbalimbali za Tanzania Bara, ikiwemo Mikoa ya Dar es Salaam, Shinyanga, Tanga, Kigoma, na Katavi.

### *Ndoa za utotoni*

- Zaidi ya miaka miwili tangu Mahakama ya Rufani ya Tanzania itoe maelekezo ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 kufanyiwa marekebisho kuweka miaka 18 kama umri wa chini wa kuoa na kuolewa na hivyo kuondoa ndoa za utotoni, bado sheria hiyo haijafanyiwa marekebisho. Hata hivyo, mwishoni mwa mwaka 2021 Tanzania ilibainisha nia ya kufanya marekebisho hayo katika ripoti yake ambayo ilitumwa kwa ajili ya tathmini ya utekelezaji wa wajibu wake katika mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu kwenda Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu.
- Mwaka 2021 LHRC ilikusanya matukio 37 ya ndoa za utotoni, sawa na ongezeko la matukio mawili ukilinganisha na matukio yaliyokusanywa mwaka 2020. Matukio haya yaliripotiwa katika mikoa kama vile Katavi, Shinyanga, Mara, Mtwara, Lindi, Kilimanjaro, Dodoma, Kigoma, na Rukwa. Wasichana wengi waliolazimishwa kuolewa walikuwa na miaka 13 hadi 16.

*"Juzi kati kuna mama alitaka kumuoza mtoto wake aliyemaliza darasa la 7, baadae tukawa tumeshaongea na mtendaji, mama alivyoulizwa anasema mbona sisi tuliolewa wadogo"*
**Afisa Ustawi, Morogoro Manispaa**

- Mahari Ilitajwa kama sababu kuu ya wazazi, hasa wa kiume, kuwalazimisha watoto wao wa kike kuolewa. Kwa mwaka 2021, mhanga wa ndoa za utotoni mdogo kuliko wote aliyeripotiwa kuokolewa alikuwa na umri wa miaka 11. Karibu nusu ya matukio (asilimia 46) yaliripotiwa katika Kanda ya Ziwa, hasa katika Mkoa wa Mara; na Kanda ya Magharibi, hasa Mkoa wa Katavi. Wafanyaji wengi wa ukatili huu walikamatwa.

*"….kuna babu hapa Kimanzichana kazi yake kuoa watoto wa miaka 16 akiwazalisha tu anawaacha na wazazi wa watoto wanakubali ilimradi wanapata hela….."*
**Mwanajamii, Mkuranga - Pwani**

- Katika Mkoa wa Mara, ukeketaji ulitajwa kama mojawapo ya visababishi vya ndoa za utotoni miongoni mwa wasichana. Hii ni kwa sababu wasichana waliokeketwa wanachukuliwa kuwa tayari kwa ndoa na kuanzisha familia zao wenyewe.

*"…ukeketaji ndiyo changamoto sana kwenye eneo hili. Na jamii hii ina amini kuwa mtoto akikeketwa anakuwa anajiandaa na maisha ya ndoa; hivyo inapelekea watoto kuolewa wakiwa na umri mdogo na pia mimba za utotoni…"*
**Afisa Ustawi, Mara**

**Wito wa LHRC:** Serikali ichukue hatua za haraka kutekeleza hukumu/maelekezo ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania katika kesi ya Rebecca Gyumi ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 kwa kuweka miaka 18 kama umri wa chini wa kuoa na kuolewa na hivyo kuondoa ndoa za utotoni katika sheria hiyo.

### *Mimba za utotoni*

- Kwa mwaka 2021, mimba za utotoni, ambazo zilijumuisha hadi wasichana wenye umri wa miaka 13, ziliendelea kuripotiwa kwa wingi katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara. LHRC ilikusanya takribani matukio 2,166 ya mimba za utotoni katika kipindi cha Januari hadi Disemba mwaka 2021. Matukio mengi kati ya hayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Kigoma, Mwanza, Morogoro, na Shinyanga.
- Sababu zinazochangia mimba za utotoni ni pamoja na utelekezaji wa watoto; msukumo kutoka kwa watoto wa rika moja; mitandao ya kijamii; baadhi ya wazazi kuwatumia watoto kuijipatia kipato; kukosekana kwa elimu ya afya ya uzazi; watoto kutokuwa na elimu ya stadi za maisha; umaskini/ugumu wa maisha; umbali mrefu kwenda shule; wazazi kutengana; ukeketaji; malezi duni; na kutojielewa.

### *Usafirishaji haramu wa watoto*

- Usafirishaji haramu wa watoto pia ulionekana kuwa tishio kwa haki za watoto mwaka 2021. Watoto nchini Tanzania husafirishwa kiharamu kwa sababu za kufanya kazi na kutumikishwa kingono, na watoto wa kike ndiye walio katika hatari zaidi ya kufanyiwa kitendo hiki cha ukatili dhidi ya watoto. Watoto wengi wanaolengwa na wasafirishaji haramu wa binadamu ni wale walio na umri wa miaka 12 hadi 17, huku wasichana wakiwa ni takribani asilimia 74 kwa mwaka 2021.
- Mwaka 2021 LHRC ilikusanya matukio 20 ya usafirishaji haramu wa binadamu, nusu ya matukio hayo yakiwa ni ya usafirishaji haramu wa watoto. Matukio hayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Mbeya, Arusha, na Iringa.
- Matukio mengi ya usafirishaji haramu wa watoto yaliyoripotiwa mwaka 2021 yalihusisha usafarishaji kwa ajili ya kufanya kazi, usafirishaji kwa ajili ya ngono, na usafarishaji wa watoto wenye ulemavu kwa ajili ya kuomba mitaani.

## 5.3. Haki wa Watu wenye Ulemavu

Kuna mkataba maalum wa kimataifa unaolinda haki za watu wenye ulemavu,

uitwao Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu (CRPD). Haki hizo ni pamoja na haki ya usawa na kutobaguliwa, haki ya kuishi, haki ya usawa mbele ya sheria, haki ya kuwa huru na salama, haki ya kutoteswa, uhuru dhidi ya ukatili, haki ya elimu, haki ya afya na haki ya kufanya kazi na kuajiriwa. Mkataba huu umeridhiwa na Tanzania na kutungiwa Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2010. Watu wenye ulemavu wanahitaji huduma maalum zitakazowawezesha kufurahia haki za binadamu sawa na watu wengine.

Tanzania imechukua hatua mbalimbali kukuza na kulinda haki za watu wenye ulemavu,ikiwemo kutunga Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2010. Kwa mwaka 2021, wanajamii wengi walioshiriki katika utafiti wa haki za binadamu uliofanywa na LHRC (asilimia 57) walidai kwamba haki za watu wenye ulemavu zimelindwa kiasi. Hata hivyo, baadhi wa wanajamii na maafisa katika ngazi ya halmashauri waliohojiwa walisema kwamba watu wenye ulemavu wanakabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo ubaguzi katika ajira, kutopata fursa za ajira na za kiuchumi, unyanyapaa, miundombinu ya majengo isiyo rafiki, ubaguzi katika elimu, na ukatili.

*"Miongoni mwa wazazi kuna dhana potofu kwamba nikizaa mtoto mlemavu ni udhaifu, kuna watoto tuliwaibua walikuwa wamefungiwa, kuna wengine wamekuwa shuleni kusoma, tulikuwa tunawachukua na kuwarudisha nyumbani kwao hivyo wengine wanapotelea tena huko nyumbani, wengine hawapati haki yao ya msingi ya kuletwa shuleni."*
**Mwalimu wa elimu maalum, Morogoro**

*"Ndugu yangu huku kwetu ukipata mtoto mlemavu ni bora umfungie ndani maana utapewa majina mengi kama vile mchawi au mkosi".*
**Mwanajamii, Mara**

- Vitendo vya ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu ambavyo viliripotiwa mwaka 2021 ni pamoja na usafirishaji haramu na utumikishwaji; ukatili wa kingono; ukatili dhidi ya watu wenye ualbino; na utelekezaji wa watoto wenye ulemavu. Mwaka 2021 takribani watu 37 wenye ulemavu walisafirishwa kiharamu kwenda kutumikishwa jijini Dar es Salaam na mtu mmoja mwenye ualbino (mtoto) aliuwawa kikatili mkoani Tabora.

*"Wakati mwingine watu wenye ulemavu, hasa wale ambao hawawezi kuongea au kusikia, hufanyishwa kazi na kisho kulipwa fedha kidogo na tofauti na kiasi walichokubaliana na watu waliowapa kazi. Kwa mfano, kuna mtu mmoja mwenye ulemavu alifanya kazi ya kupalilia na kisha akalipwa Shilingi 2,000 pekee, kinyume na makubaliano.."*

**Mfanyakazi katika shirika la haki za watu wenye ulemavu, Tanga**

- Watu wenye ulemavu, hasa watoto wenye ulemavu, pia wapo katika hatari ya kufanyiwa aina tofauti za ukatili wa kingono, ikiwemo ubakaji na ulawiti. LHRC ilikusanya matukio matatu ya ukatili wa kingono dhidi ya watu wenye ulemavu, ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mara, na Arusha.
- Japokuwa matukio ya watu wenye ualbino kushambuliwa yamepungua katika miaka ya hivi karibuni, mwaka 2021 kuliripotiwa tukio moja la mtoto mwenye ualbino kushambuliwa na kuuwawa. Hivyo, watu hawa wameendela kuishi kwa wasiwasi kiasi na kuchukua tahadhari kwa hofu ya kushambuliwa, jambo ambalo ni tishio kwa haki zao kama binadamu, ikiwemo haki ya kuishi na haki ya kuwa huru na salama. Mkoani Tanga, iliripotiwa kwamba watu wenye ualbino wilayani Handeni walioomba Serikali iwalinde ili kuweza kushiriki katika shughuli za kimaendeleo bila hofu, wakidai kwamba bado kuna watu katika jamii ambao wanataka kuwadhuru.

## 5.4. Haki za Wazee

Tofauti na makundi mengine maalum kama vile wanawake, watoto na watu wenye ulemavu, hakuna mkataba wa kimataifa wa haki za binadamu maalum kwa ajili ya wazee. Kwa hapa nchini hakuna pia sheria ya kuwalinda wazee, japokuwa Zanzibar ipo. Katika Utafiti wa Haki za Binadamu uliofanywa na LHRC mwaka 2021, zaidi ya nusu ya wanajamii walioshiriki katika utafiti huo walidai kwamba haki za wazee zimelindwa kiasi. Hata hivyo baadhi ya wanajamii, wakiwemo wazee, waliohojiwa walisema kwamba wazee wanakabiliana na changamoto mbalimbali, ikiwemo upatikanaji/ufikiaji wa huduma bora za afya, ukatili, na kukosa ulinzi/hifadhi ya kijamii.

- Changamoto wanazokabiliana nazo wazee katika kufikia huduma za afya ni pamoja na hospitali au vituo vya afya kuwepo zaidi katika maeneo ya mijini, mbali na mahala wanapoishi; gharama za usafiri; kutoweza kumudu ada za huduma au madawa; kutokuwa na taarifa sahihi kuhusu huduma na stahiki

zao; baadhi ya wafanyakazi katika sekta ya afya kutokuwa na mafunzo ya yamna ya kuwapatia huduma ya afya wazee; na mitazamo hasi kuhusu wazee miongoni mwa baadhi ya wafanyakazi katika sekta hiyo.

- Ufikiaji wa huduma za afya ulitajwa kama changamoto kwa wazee katika mikoa yote iliyofikiwa wakati wa utafiti.

*"Utekelezaji wa utoaji wa huduma bure unaenda vizuri ila kwenye dawa unaambiwa dawa haipo, mzee anaambiwa akanunue inakuwa tatizo ukimwambia akanunue ni kama umemwambia ondoka uende kufa na hili linasikitisha kweli kweli"*
**Mfanyakazi shirika la haki za wazee, Morogoro**

- Mwaka 2021 LHRC ilikusanya takribani matukio 16 ya ukatili dhidi ya wazee, ikiwemo ukatili wa kimwili, ukatili wa kingono, na utelekezaji. Matukio haya ni mara mbili ya yale yaliyokusanywa na LHRC mwaka 2020.
- Mwaka 2021 wazee pia walifanyiwa ukatili wa kimwili kwa sababu tofauti, ikiwemo kuhisiwa au kutuhumiwa kuwa wachawi na migogoro ya urithi. Watoto wa wazee hao, hasa wa kiume, walitajwa zaidi kama wafanyaji wa vitendo hivyo vya ukatili wa kimwili kwa wazee (wazazi wao).

*"Wazee wanatuhumiwa ni wachawi, wanafyekwa mapanga, kuchukua hatua immediately kuhusu masuala haya inakuwa ngumu serikali haiamini uchawi na wengine wanaogopa uchawi hivyo wanaoumia ni wazee"*
**Mkurugenzi – Shirika la Wazee Morogoro - Morogoro**

- Hali kadhalika, mwaka 2021 LHRC pia ilikusanya matukio mawili ya ukatili wa kingono dhidi ya wanawake wazee, ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Iringa na Mara.
- Baadhi ya watoto walituhumiwa kuwatelekeza wazazi wao wazee kwa kutowapatia msaada wa kifedha ili kuweza kupata mahitaji muhimu katika mikoa yote iliyofikiwa wakati wa utafiti wa haki za binadamu, ikiwemo Arusha, Katavi, Mara, and Mbeya.
- Wazee waliohojiwa katika baadhi ya mikoa, kama vile Dar es Salaam, Rukwa na Kagera, walilalamika pia kuhusu watoto wao kuingilia haki yao ya kumiliki mali, ikiwemo kwa kuwalazimisha kuwapatia 'urithi.' Hali hii imekuwa ikisababisha ugomvi na kutokuelewana, hivyo wakati mwingine kupelekea kufanyika vitendo vya ukatili dhidi ya wazee, ikiwemo mauaji. Mwaka 2021, LHRC ilikusanya matukio mawili ya wazazi kuuwawa na

watoto wao sababu ya urithi wa mali, ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Geita na Rukwa.

*"Ukatili kwa wazee upo kila mahali, watoto ndio wakatili sana kwa wazee wao, wanaweza kuwakatili mali, mashamba na hata pesa au kufanya mauaji ili wapate mali"*
**Mwanajamii - Morogoro**

*"Eneo la wazee hawajalifanyia kazi sana. Wazee wana shida sana. Wanadhulumiwa ardhi, wananyang'anywa pia mifugo na huwa wanapigwa na vijana. Wazee akina mama wanadhulumiwa kwenye suala la mirathi na taarifa hizi huwa hazifikishwi.."*
**Mwanajamii, Bukombe - Geita**

- Baadhi ya washiriki wa utafiti waliohojiwa, wakiwemo wazee, walisema kwamba kumekuwa pia na tabia ya baadhi ya watoto kuwaachia wajukuu na wao kuendelea na maisha yao, hiyvo kulazimika kuwa 'wazazi kwa mara ya pili' na kuwalea wajukuu hao bila msaada kutoka kwa watoto wao.

*"….Ndugu yangu mimi nimesomesha mtoto wangu wa kwanza wa kiume lakini hajawahi nitumia hata shilingi miamoja na kinachonisikitisha zaidi amenitelekezea mke na watoto wake yaani mimi ndio ninahangaika kuwatafutia wajukuu na mkwe wangu wale chakula yeye yupo mkoani anakula maisha."*
**Mwanajamii - Mara**

- Ulinzi wa kijamii, ambao ni muhimu sana kwa wazee, pia umeendelea kuwa changamoto. Hili lilibainishwa katika utafiti wa haki za binadamu, ambapo kukosekana kwa pensheni ya wazee kulitajwa kama mojawapo ya changamoto kubwa kwa wazee.

*"Kukosekana kwa utaratibu (system) au njia ya kitaifa ya utoaji wa wa pension ya jamii kwa wazee kwani Tanzania bado haijawa suala la kutekeleza, labda kwa Zanzibar tayari. Hata ikiwa watatoa pension ya elfu 20 ni nyingi sana, italeta manufaa mzee atanunua chumvi, kiberiti, mafuta ya taa kwa ajili ya kibatari chake"*
**Mkurugenzi - Shirika la Wazee Morogoro - Morogoro**

## 5.5. Haki za Watu waonaishi na VVU

Kwa mwaka 2021, unyanyapaa na ubaguzi viliendelea kuwa changamoto kuu kwa watu wanaoishi na VVU, hali ambayo imekuwa ikisababisha washindwe kufurahia vizuri haki zao kama binadamu. Vitendo vya unyanyapaa na ubaguzi hufanyika katika maeneo mbalimbali, ikiwemo nyumbani,

shuleni, na mahala pa kazi. Iliripotiwa mkoani Kagera kwamba baadhi ya wazazi ambao wana watoto wenye VVU waliwazuia watoto hao kwenda shule kwa sababu 'wanaweza kufa muda wowote.

**Wito wa LHRC:** Wanajamii wanatakiwa kujiepusha na vitendo vya ubaguzi au unyanyapaa wa watu wanaoishi na VVU na kuheshimu haki zao kama binadamu. Pia, kuna haja ya kuongeza juhudi za kushughulikia ukatili wa kingono dhidi ya wanawake na watoto pamoja na mimba za utotoni ili kuzuia maambukuzi mapya ya VVU miongoni mwa wanawake na wasichana.

## 5.6. Haki za Wakimbizi

Kwa miaka mingi, Tanzania imekuwa mojawapo ya nchi ambazo zimekuwa zikiwakaribisha wakimbizi kutoka nchi jirani, jambo ambalo limeipatia nchi sifa kubwa katika jumuiya ya kimataifa. Kukosekana kwa utulivu wa kisiasa katika nchi jirani kama Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwa miaka mingi, kumeifanya Tanzania kuwa kama nyumbani kwa pili kwa wakimbizi na watu wanaotafuta hifadhi. Mwaka 2021, suala kuu kwa upande wa wakimbizi waliopo nchini Tanzania lilikuwa ni madai ya kuwarudisha kwa lazima nchini kwao wakimbizi kinyume na sheria za kimataifa, hasa wakimbizi wa Burundi.

## 5.7. Haki za Vijana

Kama ilivyo kwa binadamu wengine, vijana pia wanatakiwa kufurahia haki za binadamu kama zinavyotajwa na kulindwa katika vyanzo mbalimbali vya kimataifa na kikanda vya haki za binadamu, ikiwemo Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu la mwaka 1948; Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966; Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981; na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa mwaka 1990. Kama ilivyo kwa mabara mengine, kuna mkataba maalum wa haki za vijana barani Afrika, unaoitwa Mkataba wa Vijana wa Afrika wa mwaka 2006. Kwa mujibu wa mkataba huu, vijana ni watu wenye umri wa miaka 15 hadi 35.

Nchini Tanzania, hatua mbalimbali zimechukuliwa kukabiliana na changomoto mbalimbali za vijana na kukuza haki zao. Kwa mwaka 2021, mojawapo ya hatua muhimu zilizochukuliwa ni kutengenezwa na kupitishwa kwa AJENDA YA KITAIFA YA KUWEKEZA KATIKA AFYA NA MAENDELEO YA VIJANA BALEHE (2021/22- 2024/24). Hata hivyo, bado juhudi zaidi zinahitajika kutatua changamoto mbalimbali ambazo vijana wanakumbana nazo, ikiwemo uelewa mdogo kuhusu afya ya uzazi na haki za afya ya uzazi; mila zenye madhara kama vile ukeketaji na ndoa za utotoni; usafirishaji

haramu; kutokuwa na ajira na ajira stahiki; umaskini; ajira kwa watoto na utumikishwaji wa watoto; na afya ya akili.

## 5.8. Athari ya Uviko19 kwa Haki za Makundi Maalum

Kwa mwaka 2021, LHRC iligundua kwamba kwa ujumla makundi maalum yaliathiriwa zaidi na janga la Uviko19. Miongoni mwa athari ya janga hilo kwa makundi hayo ni pamoja na kuongezeka kwa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto; wanawake kuwa katika hatari zaidi ya kufanyiwa aina tofauti za ukatili; na upotevu wa ajira/kipato. Changamoto nyingine, ambazo zilionekana kuwa tatizo kiasi na kuchangiwa na Uviko19, ni pamoja na ukeketaji, ndoa za utotoni, mimba za utotoni, na upatakanaji wa taulo za kike.



06

SURA YA SITA:

# MIFUMO YA ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU

SURA YA SITA:

# MIFUMO YA ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU


## Utangulizi

Mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu inajumuisha sheria zinazolinda haki za binadamu na taasisi mbalimbali ambazo zina jukumu la kusimamia sheria hizo na kulinda na kuimarisha haki za binadamu. Kuna mifumo ya kitaifa, mifumo ya kikanda na mifumo ya kimataifa.

## 6.1. Mifumo ya Kitaifa ya Ulinzi wa Haki za Binadamu

Mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu nchini Tanzania inajumuisha vyombo kama vile Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mhimili wa Mahakama, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Jeshi la Polisi Tanzania, na Jeshi la Magereza.

Kwa mwaka 2021, mifumo ya kitaifa ya haki za binadamu iliendelea kuchukua hatua mbalimbali kukuza na kulinda haki za binadamu. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na: kuboresha utoaji haki (Mhimili wa Mahakama); kuwakamata watuhumiwa wa ukiukwaji wa haki za binadamu na kuwafikisha mahakamani (Jeshi la Polisi); kupokea malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu na kuyafanyia kazi (Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora); uendeshaji wa mashtka dhidi ya watuhumiwa wa ukiukaji wa haki za binadamu (Ofisi ya Taifa ya Mashtaka); na kuzuia na kupambana na rushwa (TAKUKURU). Kwa upande




*Alama ilizopata Tanzania katika Utafiti kuhusu Mitazamo ya Rushwa kuanzia mwaka 2015-2021*


wa mapambano dhidi ya rushwa, Utafiti kuhusu hali ya rushwa duniani uliofanywa na Shirika la Transparency International kwa mwaka 2021 ulionyesha Tanzania kuendelea kupiga hatua katika mapambano hayo kwa kupanda zaidi katika nafasi, kutoka nafasi ya 94 mwaka 2020 hadi nafasi ya 87 mwaka 2021, baada ya kupata alama 39, ambazo ni alama moja zaidi ukilinganisha na mwaka 2020.

Pamoja na juhudi mbalimbali zilizofanyika, mifumo ya kitaifa ya ulinzi wa haki za binadamu iliendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali mwaka 2021, ikiwemo upungufu wa wafanyakazi, haki za watuhumiwa kutoheshimiwa, rushwa, ucheleweshaji katika chunguzi na kesi, na bajeti isiyotosheleza/finyu.

## 6.2. Mifumo ya Kikanda na Kimataifa ya Ulinzi wa Haki za Binadamu

Mwaka wa 2021 ulikuwa wa kipekee kwa Tanzania kwa kuwa jumuiya ya kimataifa ilifanya tathmini ya utekelezaji wa haki za binadamu nchini Tanzania kulingana na wajibu wa Serikali katika mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu. Rekodi ya haki za binadamu ya Tanzania ilifanyiwa tathmini kwa mara nyingine na Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu (tathmini ya UPR) mnamo tarehe 5 mwezi Novemba mwaka 2021. Wajumbe wa nchi 92 walitoa mapendekezo ya kuboresha ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu nchini Tanzania. Tanzania iliunga mkono asilimia 43 ya Mapendekezo yaliyotolewa, ilipokea asilimia 52 ya Mapendekezo, na iliahidi kufanyia tathmini asilimia 5 ya Mapendekezo.

Mapendekezo ya UPR kwa Tanzania 2021





07


SURA YA SABA:

# UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO KATIKA RIPOTI ZILIZOPITA ZA HAKI ZA BINADAMU

## SURA YA SABA:

# UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO KATIKA RIPOTI ZILIZOPITA ZA HAKI ZA BINADAMU

Mbali na kuelezea hali ya haki za binadamu nchini, ambazo zinalindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na mikataba ya kikanda na kimataifa, Ripoti za Haki za Binadamu zinazoandaliwa na LHRC hutoa mapendekezo kwa ajili ya kuimarisha haki za binadamu. Kwa mwaka 2021, LHRC ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Mapendekezo yalitolewa katika ripoti za mwaka 2015 hadi 2020.




*Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti za haki za binadamu za 2015 hadi 2020*

Jedwali hapo chini linaonyesha idadi ya Mapendekezo ambayo yametekelezwa (I), yaliyotekelezwa kiasi (PI), ambayo hayajatekelezwa (NI), na ambayo haijulikani kama yametekelezwa ua la (U).

**Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti za haki za binadamu za 2015 hadi 2020**

| Kipengele cha Haki za Binadamu | #Mapendekezo | I | PI | NI | U |
|---|---|---|---|---|---|
| Haki za Kiraia na Kisiasa | 67 | 22 | 24 | 21 | 0 |
| Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni | 44 | 13 | 18 | 12 | 1 |
| Haki za Makundi Maalum | 28 | 8 | 9 | 9 | 2 |
| Haki nyingine | 5 | 2 | 2 | 0 | 1 |
| **JUMLA** | **144** | **45** | **53** | **42** | **4** |

Mapendekezo mengi yaliyotolewa (47%) yalikuwa ni kwa upande wa haki za kiraia na kisiasa. Hii ni kwa sababu haki hizi ndiyo haki nyingi zaidi, kama zilivyoelezewa katika nyaraka mbalimbali za kikanda na kimataifa za haki za binadamu, ikiwemo mikataba. Pia, haki hizi ndizo zinazoongoza kwa kukiukwa ukilinganisha na makundi mengine ya haki za binadamu. Mapendekezo kuhusu haki za kiraia na kisiasa pia yameongoza kwa upande wa idadi ya mapendekezo yaliyotekelezwa (47%) na ambayo hayajatekelezwa (50%).

**Wito wa LHRC:** Ili kuimarisha ulinzi wa haki za msingi za binadamu, usawa wa kijamii, na ufikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, tunaisihi Serikali na wadau wengine kutekeleza mapendekezo ambayo bado hayajatekelezwa na yale ambayo hayajekelezwa kikamilifu



08

SURA YA NANE:

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO MUHIMU

# SURA YA NANE:
# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO MUHIMU

## Hitimisho

### *Haki za Kiraia na Kisiasa*

Kwa mwaka 2021 hali ya haki za kiraia na kisiasa ilidorora kiasi kwa sababu ya ukiukwaji wa haki za msingi kama vile haki ya kuishi, haki ya usawa wa mbele ya sheria, haki ya kuwa huru na salama, na uhuru dhidi ya ukatili. Kudorora kwa ufurahiaji na utekelezaji wa haki hizi pia kulichangiwa na athari za Uviko19. Mojawapo ya haki zilizokiukwa zaidi mwaka 2021 ni haki za watuhumiwa katika mfumo wa haki jinai. Sheria na kanuni zenye vifungu vinavyominya haki kinyume na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu pia ziliendelea kuwa kikwazo katika utekelezaji madhubuti wa haki za kiraia na kisiasa, hasa uhuru wa kujieleza, kukusanyika, na kujumuika.

### *Haki za Kiuchumi, Kijamii, na Kiutamaduni*

Kwa mwaka 2021, Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha utekelezaji wa haki za kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni kulingana na uwepo wa rasilimali na majukumu ya Tanzania katika mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa. Kwa upande wa haki ya elimu, utekelezaji wa sera kama vile sera ya elimu bila malipo uliendelea kuimarisha upatikanaji na ufikiaji wa elimu. Pamoja na

juhudi mbalimbali, utekelezaji madhubuti wa haki za kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni uliendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile ufinyu wa bajeti; upungufu wa wafanyakazi, hasa walimu na wafanyakazi wa sekta ya afya; upungufu wa madarasa na mabweni; upungufu wa matundu ya vyoo; ukatili dhidi ya watoto; mila zenye madhara; kutokuwa na ulinzi wa kijamii; na ukiukwaji wa haki za wafanyakazi.

### *Haki za Kiujumla*

Kwa mwaka 2021, haki za kiujumla, ambazo hutegemea utekelezaji wa haki nyingine, pia zilikabiliwa na changamoto mbalimbali, hasa kwa upande wa maendeleo ya kisiasa na maendeleo ya kibinadamu. Utekelezaji madhubuti wa haki kama vile haki ya maendeleo na haki ya kufurahia na kunufaika na rasilimali asilia/maliasili uliathiriwa na changamoto kama vile Uviko19, ikiwemo katika sekta ya utalii; rushwa; na ukwepaji wa kodi.

### *Haki za Makundi Maalum*

Makundi maalum yanajumuisha wanawake, watoto, watu wenye ulemavu, wazee, na watu wanaoishi na VVU. Makundi haya ni maalum kwa sababu yapo katika hatari zaidi ya haki zao kukiukwa, hali ambayo imepelekea kuwekewa ulinzi maalum, ikiwemo mikataba na sheria mahsusi, isipokuwa kwa upande wa wazee, ambao bado hawajapata mikataba ambayo ni mahsusi kwa ajili ya kulinda haki zao. Kwa mwaka 2021, matukio mengi ya ukatili na ubaguzi dhidi ya makundi haya yaliripotiwa. Ukatili wa kingono ulikuwa miongoni mwa changamoto kubwa kwa makundi haya.

## Mapendekezo

### *Haki za Kiraia na Kisiasa*

#### Serikali

- Kwa kuwa Tanzania ni mojawapo ya nchi ambazo hazitekelezi adhabu ya kifo, Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, itangaze rasmi kwamba imesitisha adhabu ya kifo na kufanya marekebisho ya sheria kuondoa adhabu hiyo kwenye sheria.
- Serikali kufanyia marekebisho Kanuni za Maudhui ya Mtandao za mwaka 2020 ili

ziendane na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.

- Serikali kufanyia marekebisho Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 kulingana na hukumu ya Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki ya mwaka 2019.
- Maafisa wa serikali kujizuia kuingilia uhuru wa kujieleza kinyume na sheria.
- Serikali kuunda chombo huru kitakachochunguza polisi na utendaji wao na kukuza uwajibikaji kwa maafisa wa vyombo vya dola.
- Mhimili wa Mhakama na TAKUKURU kufanya kazi kwa karibu kupambana na tatizo la rushwa katika mfumo wa haki ili kurejesha imani ya wananachi kwenye mfumo huo na kupunguza matukio ya wanananchi kujichukulia sheria mkononi. Hii pia itasaidia kulinda haki ya kupata haki.
- Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba maafisa wa polisi wanajiepusha na vitendo vya ubambikaji wa kesi na vitendo vingine vinavyokinzana na maadili ya Jeshi la Polisi.
- Serikali kuridhia na kutungia sheria Mkataba dhidi ya Utesaji na Adhabu au Vitendo vingine vya Kikatili, visivyo vya Kibinadamu, vya Kinyama na vyenye Kudhalilisha wa Mwaka 1984 (Mkataba dhidi ya Utesaji) ili kuongeza ulinzi wa uhuru dhidi ya utesaji.
- Jeshi la Polisi na mahakama kutoa dhamana kwa makosa yote yenye dhamana na kutoa dhamana hiyo kwa wakati.

## Wadau wengine

- Asasi za kiraia na mashirika ya kidini kutumia nafasi zao kukemea na kueneza uelewa kuhusu wananchi kujichukulia sheria mkononi, adhabu ya kifo, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, mashambulizi dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi na ajali za barabarani pamoja na madhara yake kwenye haki za binadamu.

## Wanajamii

- Wanajamii kuepuka kujichukulia sheria mkononi na kutafuta nafuu za kisheria katika ngazi ya juu zaidi ya mfumo wa haki pale ambapo hawajafurahishwa na hukumu ya kesi.
- Viongozi wa kidini na wa kijadi kutumia nafasi zao kukemea matukio ya

ukiukwaji wa haki za kiraia, hasa haki ya kuishi, uhuru wa kujieleza, na haki ya kutoteswa, kama sehemu ya kukuza haki hizi.

- Wanajamii kutoa taarifa na kufichua matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu kwa mamlaka husika ili kulinda haki hizo na kuhakikisha watuhumiwa wanafikishwa mbele ya vyombo vya sheria.

### *Haki za Kiuchumi, Kijamii, na Kiutamaduni*

#### Serikali

- Serikali, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, kuongeza bajeti kwenye sekta muhimu za afya, elimu, na maji ili kuongeza upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu, na maji, kulingana na viwango vya kimataifa kuhusiana na bajeti za sekta hizi, sambamba na kuhakikisha fedha zilizotengwa zinawasilishwa zote na kwa wakati.
- Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia kuongeza upatikanaji wa elimu kwa watoto wenye ulemavu (elimu jumuishi) kwa kuhakikisha uwepo wa miundombinu inayohitajika, walimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

#### Wadau wengine

- Asasi za kiraia kushirikiana na wizara husika, kama vile wizara inayohusika na masuala ya jinsia na wizara inayohusika na ardhi, katika kukuza na kulinda haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, ikiwemo kufanya kampeni za pamoja na kueneza uelewa kuhusu haki hizo.
- Asasi za kiraia kushirikiana na Wizara ya Kazi na Sheria kueneza uelewa kuhusu sheria za kazi, haki na wajibu.

#### Wanajamii

- Wanajamii kutoa taarifa kuhusu matukio ya ukiukwaji wa haki za kiuchumi kwa mamlaka husika, ikiwemo vyama vya wafanyakazi na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.
- Wazazi kufanya juhudi za kuelewa majukumu yao kuhusiana na watoto chini ya Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 na kufanya juhudi za kuhakikisha

kwamba watoto hao wanafurahia na kutekeleza haki zao, ikiwemo haki ya kupata elimu na uhuru dhidi ya ukatili.

### *Haki za Kiujumla*

#### Serikali

- Wizara ya Utalii na Maliasili kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa sheria za maliasili.
- Serikali, kupitia Kituo cha Uwezekaji Tanzania, kuhakikisha wawekezaji wanaheshimu haki za binadamu na kufuata sheria za nchi katika utekelezaji wa shughuli zao.
- Serikali kuongeza juhudi za kupambana na ukwepaji kodi, hasa katika sekta ya madini na kuhakisha makampuni yanayokwepa kodi yanawajibishwa kisheria.

#### Wadau wengine

- Asasi za kiraia na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kueneza uelewa kuhusu haki ya maendeleo na haki ya kufurahia na kunufaika na maliasili.
- Asasi za kiraia kutambua mianya katika utekelezaji wa haki ya kufurahia na kufaidika na maliasili na kuishauri Serikali ipasavyo.

#### Wanajamii

- Wanajamii wanahamasishwa kutunza na kulinda maliasili, kwani ni wajibu wao kikatiba.
- Wanajamii kuwajibika kwa kulipa kodi, jambo ambalo ni muhimu kwa utekelezaji wa haki za kijamii na kiuchumi.

### *Haki za Makundi Maalum*

#### *Serikali*

- Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, kupeleka bungeni muswada wa kutunga sheria maalum ya ukatili wa kijinsia/ukatili majumbani.
- Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Tume ya Kurekebisha Sheria, kufanya mapitio na kuondoa au kurekebisha sheria zote zinazowabagua wanawake na kuwanyima haki zao kinyume na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa iliyoridhiwa na Tanzania.

- Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Tume ya Kurekebisha Sheria, kuridhia Mkataba wa Nyongeza katika Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Watu wenye Uleamvu barani Afrika wa mwaka 2018.
- Serikali, kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kuingiza elimu ya jinsia katika mitaala ya elimu katika ngazi zote za elimu.
- Serikali, kupitia wizara za fedha na mambo ya ndani, kuongeza bajeti kwa ajili ya madawati ya polisi ya jinsia na watoto ili kuyawezesha kushughulikia vizuri vitendo vya ukatili.
- Serikali kuridhia Mkataba Namba C190 wa Shirika la Kazi Duniniani kuhusu Ukatili na Unyanyasaji Mahala pa Kazi wa mwaka 2019 ili kuongeza juhudi za kutokomeza vitendo vya ukatili na unyanyasaji mahala pa kazi.
- Serikali kutimiza wajibu wake chini ya mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa kuhusu haki za watoto na kulingana na hukumu ya Mahakama ya Rufaa kwenye kesi ya Rebeca Gyumi ya mwaka 2019 kufanya mabadiliko ya sheria ili kuondoa ndoa za utotoni kwenye Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.
- Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, kuanzisha mchakato wa kutunga sheria maalum ya kulinda haki za wazee.
- Serikali, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, kuongeza bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto, ikizingatiwa kwamba matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto yanaongezeka.

### Wadau wengine

- Asasi za kiraia na vitengo vya ustawi wa jamii kuongeza juhudi za kueneza uelewa kuhusu ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kuwahamasisha wanajamii kutoa taarifa kuhusu matukio ya namna hiyo kwa mamlaka husika ili watuhumiwa wakamatwe na kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria.
- Asasi za kiraia kuendelea kueneza uelewa kuhusu haki za makundi maalum, ikiwemo haki za wazee na kufanya kampeni za kupinga na kutokomeza ukatili na ubaguzi dhidi ya wazee.

### Wanajamii

- Wanajamii kujiepusha na vitendo vya ubaguzi dhidi ya watoto, ikiwemo watoto wa mtaani na watoto wenye ulemavu.
- Wanajamii kujiepusha na tabia ya kuwalinda watuhumiwa wa ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa sababu tu ya kutaka 'kuficha aibu ya familia.'

## *Mifumo ya Ulinzi wa Haki za Binadamu*

### *Serikali*

- Serikali kuimarisha mifumo ya kitaifa ya ulinzi wa haki za binadamu na kushughulikia changamoto ambazo mifumo hiyo inakabiliana nazo ili kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu.
- Serikali kufikiria upya maamuzi yake ya kuzuia asasi za kiraia na watu binafsi kufungua kesi dhidi ya Serikali katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.
- Serikali kutekeleza maamuzi/hukumu za Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kuhusu mgombea binafsi na adhabu ya lazima ya kifo, na hukumu ya Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki kuhusu Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016.

### Wadau wengine

- Asasi za kiraia kushirikiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kuwajengea maafisa wa vyombo vya dola uwezo kwenye masuala ya haki za binadamu na umuhimu wa kuheshimu haki hizo.
- Vyombo vya habari kuripotia kuhusu mifumo mbalimbali ya haki za binadamu na nafasi yake katika kulinda na kukuza haki za biandamu na namna inavyoweza kufikiwa na wananchi.
- Asasi za kiraia kuuelimisha umma kuhusu mifumo mbalimbali ya kitaifa, kikanda, na kimataifa ya ulinzi wa haki za binadamu.

### Wanajamii

- Wanajamii kuhamasika kuifikia mifumo mbalimbali ya ulinzi wa haki za binadamu au kufanya hivyo kwa msaada wa asasi za kiraia, pale ambapo haki zao zimekiukwa, ili kupata nafuu ya kisheria.



LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
**LHRC**
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

**Are you passionate about the protection and promotion of Human Rights?**

## Donate Now!

airtel money

### How to Donate (Airtel Money)

1st Step: Dial *150*60# to access your AIRTEL MONEY account.
2nd Step: Select 5 – Make Payments.
3rd Step: Select 4 – Enter Business Number.
4th Step: Enter business number (275454)
5th Step: Enter the amount you want to pay.
6th Step: Enter the reference number.(1234)
7th Step: Enter your “PIN” to confirm.

tigo pesa

### How to Donate (TigoPesa)

1st Step: Dial *150*01 # to access your Tigo Pesa account.
2nd Step: Select 4 – Pay Bills.
3rd Step: Select 3 – Enter Business Number.
4th Step: Enter business number (275454)
5th Step: Enter the reference number.(1234)
6th Step: Enter the amount you want to pay.
7th Step: Enter your “PIN” to confirm.

vodacom m-pesa

### How to Donate (M-PESA)

1st Step: Dial *150*00# to access your MPESA account.
2nd Step: Select 4 – Pay By Mpesa.
3rd Step: Select 4 – Enter Business Number.
4th Step: Enter Business number (275454)
5th Step: Enter the reference number.(1234)
6th Step: Enter the amount you want to pay.
7th Step: Enter your “PIN” to confirm.
8th Step: Enter 1 to confirm the transaction

@humanrightstz You Tube Haki TV

*For a Just and Equitable Society*

**LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE, HEADQUARTERS**
Justice Lugakingira House, Kijitonyama,
P. O. Box 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Tel:** +255 22 2773038/48 **Fax:** +255 22 2773037
**Email:** lhrc@humanrights.or.tz **Website:** www.humanrights.or.tz

---

**THE LEGAL AID CLINIC**
Isere Street – Kinondoni, P. O. Box 79633, Dar es Salaam, Tanzania
**Phone/Fax:** +255 22 27612015/6 **Email:** legalaid@humanrights.or.tz

---

**ARUSHA OFFICE,**
Olerian Street, Plot No. 116/5, Sakina kwa Iddi
P. O. Box 15243, Arusha, Tanzania
**Phone:** +255 27 2544187 **Email:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

---

**DODOMA OFFICE**
Plot No. Area D, P. O. Box 2289, Dodoma, Tanzania
**Phone/Fax:** +255 262350050 **Email:** lhrc@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV